

**23 SEPTEMBA, 2022**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 23 Septemba, 2022**

(Bunge Lilianza Saa Tatoo Asubuhi)

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 134

**Wastaifu ambao waajiri hawakupeleka michango kulipwa haki zao**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Je, ni lini wastaifu ambao waajiri wao walikuwa hawatoi michango katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii watalipwa haki zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mafao ya pensheni hulipwa kwa mstaafu kwa kuzingatia kipindi kilicholipiwa michango yake. Kumekuwepo na changamoto kwa baadhi ya waajiri kushindwa kuwasilisha michango ya watumishi wao katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa wakati. Kutohana na changamoto hiyo, mifuko imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwemo kuwapeleka Mahakamani waajiri ambao hawawasilishi michango kwa wakati ili kuwezesha wastaafu hao kupata haki yao.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na mifuko kukabiliana na changamoto hii ni pamoja na kutoa elimu kwa waajiri, kutengeneza namba ya kumbukumbu ya malipo (*control number*) kuitia Mfumo wa Malipo ya Serikali (*GePG*) na kupunguza tozo zinazotokana na ucheleweshwaji wa michango hiyo. Aidha, mifuko imeingia makubaliano maalum na waajiri 63 ya namna ya kulipa madeni yao.

Mheshimiwa Spika, waajiri ambao wameendelea kukaidi kuwasilisha michango ya wanachama kwa wakati, Mifuko kwa kushirikiana na Wakili Mkuu wa Serikali (*Solicitor General*) imechukua hatua ya kuwapeleka Mahakamani kwa mujibu wa sheria. Aidha, waajiri 123 tayari wamefikishwa Mahakamani, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia Wambura swali la nyongeza.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, swali langu la kwanza, je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na wale wastaafu ambao wanapigwa danadana wakati wakifutilia mafao yao ambayo ni difference au utofauti ya kile kipindi ambacho makato yamepelekwa kwenye mifuko na kile kipindi ambacho hayajapelekwa kwenye mifuko na madai ni kwamba Maafisa Masuuli wamehama au hawakupata uteuzi?

Swali la pili, ningependa kujua kama Serikali itakuwa tayari sasa kuwataka waajiri au kuwahimiza watekeleze masharti ya mifuko haraka iwezekanavyo ili wale wastaafu waweze kulipwa haki zao? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa kipindi cha nyuma kulikuwa na changamoto ya wazee wetu waliotumikia Taifa kwa nguvu zao lakini pia kwa uadilifu na utumishi uliotukuka, walikuwa wakipata usumbufu katika kupata mafao yao aidha kwa kuambiwa kuleta barua na changamoto nyingine nyingi ambazo zilikuwepo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako pamoja na mimi na wasaidizi wengine kulikuwa na mpango kabambe wa kuweza kupita katika mikoa yote, kukutana na wastaafu na kutatua changamoto hizo na zoezi hili lilifanikiwa na kwa hatua ya sasa tayari tumekwisha kuanza kutatua changamoto hizo na kama kuna specific case ambayo bado haijafanyiwa kazi, ni muombe Mheshimiwa Mbunge aweze kutufikishia ili tuchukue hatua haraka sana iwezekanavyo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la pili pia kwamba kutokana na waajiri sasa kutokutekeleza wajibu; ni tamko la Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba waajiri wote nchini wanao wajibu wa kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini lakini sambamba na hilo Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii yaani *National Social Security Fund Act* ambayo inamtaka mwajiri kuwasilisha michango ya mwajiriwa wake bila usumbufu wowote na wajibu huu upo kwa mwajiri kwa mujibu wa sheria na kama atakiuka, kama jinsi ambavyo tumefanya kwa hawa 123 kuapeleka mahakamani.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo hata mahakama kwa mujibu wa Bunge lako tukufu lilitunga sheria ambayo mwajiri ambaye atakuwa amekiuka kupeleka michango ya mwajiriwa wake akienda mahakamani anatumia procedure ya *summary suit*, kwa hiyo hana hata wajibu wa kuweza kujitetea na hatua tunachukua.

Kwahiyo, niwaombe na kuwataka waajiri wote nchini kutimiza takwa hilo la kisheria ili tusije tukafikishana mahakamani na kuchukuliwa hatua kali zinavyostahili kwa mujibu wa sheria, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, malalamiko haya ni mengi, hebu tusaidie, ni kazi ya nani kuhakikisha mwajiri anapeleka makato anayoyatao kwenye mshahara wa mfanyakazi na ile anayotakiwa kulipa yeye kuhakikisha inafikia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; ni kazi ya nani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa swalii zuri; kwa mujibu wa sheria ambayo ilipitishwa na Bunge lako tukufu Sheria ya *National Social Security Fund* inasema wajibu ni wa mwajiri kufikisha, lakini sambamba na hilo ni wajibu wa mfuko pia kuweza kufanya ufuatiliaji wa michango hiyo kuhakikisha inafikishwa. Kwa hiyo ni pande zote mbili; mwajiri anao huo

wajibu kwa mujibu wa sheria lakini mchango wanao ma-compliance officer kwa mujibu wa sehria katika utekelezaji nao NSSF au PSSF au mifuko hii ya hifadhi inapaswa kuendelea kumkumbusha mwajiri na kumpa notice. Na kwa sasa tayari kumekwishachukuliwa utaratibu wa kufungua akaunti ya kimtandao ya moja kwa moja, kila mwanachama sasa anapewa taarifa yake kupitia simu ya kiganjani. Kwa hiyo, kama michango haiendi kwa sasa tunawakamata.

Mheshimiwa Spika, kwa hili kwa kweli tunaendelea na operation kali kuweza kufanya ukaguzi ili kuweza kuhakikisha takwa hili la kisheria linatimia na wastaafu wetu wasisumbuliwe. Ahsante.

**SPIKA:** Nawaona Waheshimiwa nataka kwenda nalo vizuri, kwa sababu Ofisi za Wabunge zina malalamiko mengi sana ya wastaafu wa nchi hii na tukisema kwamba tutaliacha liendelee mtu anafuatilia mafao miaka miwili anaambiwa michango yako haikuja, kama ni kazi ya mwajiri kupeleka na mfuko unajua mwajiri hajapeleka, ni kazi yao, mfuko umlipe huyu mafao yake wao wakatafute fedha zilipo kwa sababu sio kazi yangu mimi kama mwajiriwa kuanza kusema fedha kama zilikuja ama hazikuja sio kazi yangu halafu huyu mwajiri mimi naweza kumuadhibu asipopeleka? Siwezi. Kwa hiyo, ni kazi ya mifuko kufuatilia fedha ambazo hazijalipwa na ndio maana sheria imeweka isipolipwa kuna riba inayotakiwa kulipwa.

Kwa hiyo, sidhani kama wananchi wanatakiwa kuteseka baada ya kuwa wamelipa kwenye mifuko na mwajiri ameshakata fedha. Ninyi Serikali mtengeneze utaratibu mzuri wa kuisimamia mifuko izitafute hizo fedha iwalipe wastaafu, wasataafu wasiwe wanaseka. (Makofii)

Waziri nakuona umesimama, nadhani tutapata tamko zuri hapo ili wastaafu wetu wawe na utulivu. Ahsante sana karibu Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kuhusiana na hatua ambazo Serikali inafanya kuhakikisha kwamba wastaafu ambao wamelitumikia Taifa letu kwa uadilifu mkubwa hawapati usumbufu wa kupata mafao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto ya baadhi ya waajiri kutopeleka michango yao katika mifuko na hivyo kusababisha wasataafu ambao michango haikupelekwa ama kutopata mafao yao kwa wakati au kupata mafao ambayo yana mapunjo.

Mheshimiwa Spika, nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba Serikali imeliona suala hili na tunalifanyia kazi ili kuweza kupata ufumbuzi kwa wale

**23 SEPTEMBA, 2022**

waajiri ambao madeni yao yameshakuwa ya muda mrefu yako ambayo yanafika miaka kumi, bado hajaleta hizo fedha.

Kwa hiyo, nilihakikishie Bunge lako kwamba tayari Serikali inafanya kazi, na niahidi kwamba ndani ya miezi miwili mitatu, tutakuja na muafaka wa kutatua tatizo hili ambalo limekuwa la muda mrefu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana, kwa majibu hayo. Miezi mitatu nadhani lile Bunge la mwezi wa kwanza tutakuwa tukipata majibu haya. Kwa hiyo, tunakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa hilo.

Waheshimiwa Wabunge, niliwaona mmesimama lakini nadhani maswali kwenye hoja hii yameshajibowi kikamilifu kabisa.

Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 135

**Waajiri wanaosuasua katika kuwaajiri watu  
wenye ulemavu nchini**

**MHE. KHADIJA S. TAYA** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa waajiri ambao wanaosuasua katika kuwaajiri watu wenyе ulemavu wenyе sifa stahiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu, Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa niaba ya Wazir Mkuu naomba kujibu swali namba 135 liloulizwa na Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2010, Serikali ilitunga Sheria ya Watu wenyе Ulemavu Na. 9 kwa lengo la kusimamia masuala mbalimbali ya watu wenyе ulemavu. Katika kifungu cha 31(1) kinaeleza kuwa kila mwajiri wa umma au binafsi, endapo kutatokea nafasi ya ajira na mtu mwenye ulemavu aliyekidhi viwango vya chini vya ajira hiyo akaomba atalazimika kumwajiri. Aidha, kifungu 31(2) cha Sheria ya Watu wenyе Ulemavu Na. 9 ya 2010 kinaeleza kuwa kila mwajiri mwenye waajiriwa kuanzia 20 na kuendelea anatakiwa kuwa na watu wenyе Ulemavu wasiopungua asilimia tatu ya waajiriwa wake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia takwa hili la sheria naomba kuwakumbusha waajiri wote kuzingatia viwango hivyo vya ajira kama vilivyoelekezwa katika sheria na tutaendelea kufanya kaguzi na kuchukua hatua kwa wasiotekeleza takwa hilo la msingi la kisheria na kibinadamu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Taya, swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita, imeanzisha vyuo vya watu wenye ulemavu, kati ya mafunzo ambayo wanayotoa pale mojawapo ni kutengeneza viatu na hapo hapo katika Wizara hii hii wamefungua kiwanda cha kutengeneza viatu pale magereza Mkao wa Kilimanjaro; je, katika hiki kiwanda walemvu wameajiriwa na kama wameajiriwa ni wangapi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ikiwa takwimu unazo unaweza kumjibu sasa, kama takwimu huna unaweza kumpatia Mheshimiwa Mbunge baadaye kwa sababu kanuni zinakuruhusu. Karibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, kwa kuthibitisha *spirit* ile ile ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan katika utekelezaji mzuri wa sheria hii ya watu wenye ulemavu, katika kile kiwanda ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja zoezi bado kwanza kiko katika hatua ya awali ya kuanza kufanya *mobilization* na ukamilishaji wa ujenzi bado haujatimia.

Mheshimiwa Spika, lakini katika uthibitisho wa hilo kwamba tunazingatia hili kama Serikali, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kuratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu katika nafasi za walimu 8,000 zilizotoka mwaka 2020 watu wenye ulemavu 242 walijiriwa ambao ni asilimia 3.2. Sambamba na hiyo katika nafasi za mwaka 2021 za walimu zilizotolewa zilikuwa nafasi 6,949 watu wenye ulemavu 145 walijiriwa ambao ni sawa na asilimia mbii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo pia mwaka 2022 katika usimamizi na utekelezaji mzuri wa Serikali ya Awamu ya Sita, ajira zilizotolewa 9,800 za nafasi ya walimu watu wenye ulemavu 261 walipata sawa na asilimia 2.66. Katika sekta ya afya na maeneo mengi sababu ya muda nafasi 7,612 ambazo zilitolewa watu wenye ulemavu waliopata nafasi hiyo ni 0.63 kulingana na sifa na vigezo ambavyo viliwekwa.

Mheshimiwa Spika, katika Serikali hii tumeweka *minimum standard*, kwamba hata vile viwango vya ufaulu tunaviangalia katika hali ambayo yule anakuwa sifa kwa sababu watu wenye ulemavu wanakuwa wachache katika uombaji wa nafasi hii.

Kwa hiyo, tutaendelea kuzingatia sheria na kuhakikisha kwenye private sector na Serikali tunazingatia takwa hili la kisheria la kuajiri watu wenye ulemavu, kwa sababu kufanya hivyo pia ni ibada kwa nchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 136

**Gari la kubebea wagonjwa Kituo cha Afya Gidas - Babati**

**MHE. DANIEL B. SILLO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la kubebea wagonjwa katika Kituo cha Afya Gidas?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji mkubwa uliopo wa magari ya kubebea wagonjwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali kuitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVICO-19 imefanya manunzi ya magari 195 ya kubebea wagonjwa ambayo yatapelekwa kwenye Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Babati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Baran Sillo.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza kwa kuwa magari yaliyonunuliwa ni 195 na halmashauri ziko 184 nchini; je, kati ya haya magari yaliyobaki moja litakwenda kwenye Kituo cha Afya cha Gidas?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa mahitaji ya wahudumu wa afya katika kituo hicho ni 32 na waliopo sasa ni nane tu; je, Serikali iko tayari kuongeza wahudumu wa afya ili kuboresha huduma za afya kwenye kituo hicho? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijiini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba magari yatakayonunuliwa ni 195 lakini tuna halmashauri 184 na tutazama zile halmashauri au vituo ambavyo viko mbali zaidi maeneo ambayo ni *hard to reach* tutawapa kipaumbele kuwapa gari zaidi ya moja katika halmashauri hizo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hoja ya Kituo cha Afya cha Gidas amesema kwa muda mrefu, tutakwenda kuona uwezekano wa kuwatafutia gari ili tuweze kuondoa changamoto ya wananchi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, kuhusiana na watumishi ni kweli tunachangamoto ya upungufu wa watumishi, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo ameona Serikali imeendelea kuajiri watumishi na kuapeleka kwenye vituo vya afya, tutahakikisha tunaendelea hivyo kwa awamu na tutaoa kipaumbele cha afya hicho cha Gidas. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, na matatizo ya magari ya kubeba wagonjwa katika vituo vya afya; je, ni lini Serikali itapeleka magari hayo katika Kituo cha Afya cha Kisolya na kile cha Kasuguti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Charles Kajege, Mbunge wa Jimbo la Mwibara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, magari ya wagonjwa yatapeleka kwenye halmashauri zote 184 nchini kote na sasa ni maamuzi ya halmashauri kuona

kipaumbele katika halmashauri yao ni kituo kipi cha afya ambacho kina uhitaji zaidi wa gari la wagonjwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Arumeru kuna gari moja tu la kubebea wagonjwa; je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka gari la ziada katika Wilaya ya Arumeru?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun Swai, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kati ya Oktoba na Novemba mwaka huu gari moja jipya la wagonjwa litapelekwa katika Halmashauri hii ya Arumeru. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kuna halmashauri ambazo zina hospitali mbili za wilaya ikiwemo na halmashauri ninayotoka mimi ya Geita. Sasa Serikali itapeleka magari mawili kwa sababu ukipeleka gari moja linakuwa na mgongano wa hoja kwa sababu kuna hospitali mbili na Wabunge wawili tofauti.

Je, Serikali ipo tayari kupeleka magari mawili katika Halmashauri ya Geita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma Mbunge wa Jimbo la Geita Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, magari yanapelekwa kwenye halmashauri na halmashauri ziko 184 magari yako 195. Kwa hiyo, kila halmashauri ikiwepo halmashauri ya Mji wa Geita lakini pia Halmashauri ya Wilaya ya Geita watapata gari moja moja, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kumekuwa na ahadi ya muda mrefu sana kupeleka gari ya wagonjwa katika Kituo cha Afya Mlola. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo kupeleka gari Kituo cha Afya Mlola?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Shabani Shekilindi, Mbunge wa Jimbo la Lushoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, halmashauri ya Lushoto itapewa gari la wagonjwa jipya kati ya Oktoba na Novemba mwaka huu, kwa hivyo nimuombe Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Mkurugenzi waone uwezekano wa kupeleka gari hili katika kituo cha afya cha kipaumbele kikubwa zaidi ikiwemo hicho ambacho amekitaja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge swalii la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kutokana na umbali wa Kituo cha Afya Nanjilinji kutoka Makao Makuu ya Wilaya, lakini pia kutoka Hospitali ya Wilaya ya Kinyonga; je, Serikali itakubaliana nami kwamba upo umuhimu wa kupeleka gari la wagonjwa kwa umuhimu wake na upekee wake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Ally Kassinge, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikweli Kituo cha Afya Nanjilinji kiko mbali lakini kinahudumia wananchi wengi na Mheshimiwa Mbunge amekifuatilia na tumekubaliana kwamba katika vituo ambavyo vitapewa magari ni pamoja na Kituo cha Afya cha Nanjilinji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga swalii la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Simbayi na Tarafa ya Basuto katika Jimbo la Hanang tuna changamoto kubwa sana kwanza ya umbali na hakuna gari

la wagonjwa; je, ni lini Serikali sasa itapeleka magari ya wagonjwa katika maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarafa hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja alikwishazileta na pia kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge Hhayuma wamekuwa wakishirikiana kwa karibu sana na kuona wananchi wa Hanang wanapata huduma hizi na nimhakikishie tu kwamba Mheshimiwa Mbunge tumeshafanya tathinini ya kuona uwezekano wa kupeleka la wagonjwa lakini gari moja la wagonjwa jipya litaletwa Hanang ili muweze kupeleka katika tarafa hizo, ashante.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalumu sasa aulize swalii lake.

Na. 137

**Kuweka vifaa vya utambuzi katika masoko, shule na sehemu zenyenye mkusanyiko**

**MHE. LUCY J. SABU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka CCTV camera na alarm systems katika masoko, shule na sehemu za wazi zenyenye mkusanyiko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti majanga mbalimbali katika taasisi, Serikali imekwishachukua hatua mbalimbali ambapo kupitia Mpango wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati Tanzania na Mpango wa Uboreshaji wa Miji jumla ya miji 26 iliyotekeleza miradi ya kimkakati ya ujenzi wa masoko, stendi, na bustani za kupumzikia zimefungiwa vifaa vya utambuzi ikiwemo CCTV camera na alarm system. Aidha, ukarabati wa shule 89 kongwe na chakavu

uliofanyika umezingatia miundombinu ya kujikinga na majanga hususani majanga ya moto.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishatoa maelekezo katika Mikoa yote nchini kuzingatia ufungaji wa vifaa vya kutambua na kudhibiti majanga mbalimbali katika taasisi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy John Sabu swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa teknolojia inabadilika kila wakati; je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa hizo CCTV camera na alarm systems zinahuishwa kila wakati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikali imeshachukua hatua ya kuanza kufunga mifumo ya kutambua na kudhibiti majanga kwa majengo mapya; je, Serikali inatoa kauli gani kwa majengo ya zamani? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumeshaweka mpango wa kitaifa wa kudhibiti majanga hususani majanga ya moto na tayari tumeshaanza kufanga katika maeneo hayo na tunafahamu kwamba teknolojia ni *dynamic*, inabadilika mara kwa mara na sisi tumejipanga kuhakikisha tunahuisha mifumo hii ya udhibiti lakini pia ya kutambua changamoto za majanga ikiwepo moto kila mara.

Kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze kwa ufuutiliaji wake mzuri kwamba Serikali imeweka mfumo ambao utakuwa mara kwa mara unapitia na ku-update mifumo hiyo ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu majengo ya zamani ni kweli kwamba mifumo hii sasa kwenye majengo mapya imekuwa sehemu ya michoro kuhakikisha kwamba inazingatia uwepo wa vifaa na miundombinu hiyo. Lakini tumetoa maelekezo katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika mikoa kote nchini kuhakikisha katika majengo yale ya zamani yakiwemo masoko,

Ofisi za Serikali na maeneo kama hayo wanafunga mifugo ya kutambua na kudhibiti majanga ya moto, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Edwin enosy Swalle Mbunge wa Lupembe sasa aulize swali lake.

Na. 138

**Kuteua Majaji wa muda kusikiliza kesi za mauaji**

**MHE. EDWIN E. SWALLE** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Serikali isiteue Majaji wa muda mfupi (*Acting Judges*) ili kusikiliza kesi za mauaji zinazochukua muda mrefu Mahakamani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo na Makazi kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y.  
WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa Majaji upo Kikatiba. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haina ibara inayotambua au kuruhusu uteuzi wa Majaji wa muda mfupi (*Acting Judges*). Aidha, Ibara ya 117(3) ya Katiba inatambua uwepo wa Mahakimu wenyewe mamlaka ya nyongeza ya kusikiliza baadhi ya mashauri ya Mahakama Kuu yakiwemo kesi za mauaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante .... Nyongeza. Swali la kwanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Swalle rejea tena maelezo uliyoyatoa mwanzo kwa sababu ulikuwa hujawasha kisemeo.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza; swali la kwanza kwa kuwa watuhumiwa wengi wanakaa muda mrefu mahabusu na kesi zao zinachelewa kwa sababu ya upelelezi.

Ni lini Serikali italeta sheria Bungeni kuweka ukomo wa makosa ya jinai?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili kwa kuwa makosa mengi ambayo watu wanakaa muda mrefu kwenye mahabusu hayana dhamana; ni lini Serikali italeta Bungeni sheria ili kuruhusu makosa yote kuwa na dhamana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y.**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bunge lako limekuwa linafanya marekebisho ya mara kwa mara ya sheria zetu hasa zile zinazohusu *Penal Laws* na *Criminal Procedure Act* ambayo kwa kumbukumbu nzuri Mheshimiwa Mbunge katika Bunge la mwezi Februari moja ya sheria inayohusu upelelezi ililetwa hapa katika mabadiliko madogo ya sheria na yako mabadiliko tuliyoyafanya ikiwemo kuruhusu sasa upeleleze ukamilike kwanza kabla kesi hazijapelekwa mahakmani.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo Katiba ya Jamhuri ya Muungano katika Ibara ya 13 katika issue za *presumption of innocence* nayo pia imesisitiza juu ya kuwepo kwa haki jinai ambazo zinataka mtu asiukumiwe kwanza isipokuwa kila mtu mbele ya sheria aonekane si mkosefu mpaka pale mahakama itakapodhibitisha jambo hilo.

Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na kuhakikishia Bunge lako lote kwamba Serikali chini ya uongozi wa Rais wetu mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan imeendelea kufanya mabadiliko ya sheria ili kukidhi haki ya jinai kama ambavyo umetaka ifanyiwe marekebisho.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 139

**Serikali kupitia upya Mfumo wa Haki Jinai**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupitia upya mfumo wa haki jinai ili kupunguza changamoto ya idadi kubwa ya mahabusu kuliko wafungwa magerezani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y.  
WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria naomba kumjibu Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha maboresho ya mfumo wa haki jinai nchini yanafanyika ili kuimarisha upatikanaji wa haki jinai nchini ikiwemo kuondokana na mlundikano wa mahabusu katika magereza yetu. Kutokana na umuhimu huo, Wizara imeandaa andiko la mapendekozo ya maboresho ya mfumo wa haki jinai ikishirikiana na Taasisi Zisizo za Kiserikali, Taasisi za Dini na Vyuo vinavyotoa elimu ya sheria ili kuhakikisha kwamba Mfumo wa Haki Jinai unafanyiwa marekebisho na kuwekwa sawa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali nakuona umesimama.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Ardhi kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria ningependa kurejesha kumbukumbu sahihi za kazi ya Bunge hili kwamba Sheria Namba 1 ya mwaka 2022 iliyotungwa na Bunge hili mwezi wa pili ilizuia kufikishwa mahakamani kwa kesi ambazo upelelezi bado isipokuwa kwa makosa yale makubwa. Hiyo ni hatua moja kubwa sana na iliyolenga kupunguza msongamano wa mahabusu. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na Mwanasheria Mkuu natambua kwamba mwaka jana tulibadilisha sheria ya kuzuia ukamataji kabla ya kukamilisha upelelezi, lakini jambo hili bado halitekelezeki na ndiyo maana hata hivi karibuni Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amelisemea na amelitolea maelekezo; kwa mantiki hiyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, Serikali haioni umuhimu wa kurekebisha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai (CPA) ili kuweka ukomo

wa upelelezi kama ambavyo wenzetu wa upande wa Zanzibar wamefanya na nchi jirani za Kenya, Uganda, Malawi na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka masharti nafuu ya dhamana kwa watu ambaa hawana mali kwa sababu hivi sasa masharti ya dhamana ni makubwa kuliko makosa hivyo ni kana kwamba tunakomoa wananchi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Neema Lugangira swalii lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya msingi wakati najibu swalii la Mheshimiwa Enosy Swalle nilieleza hatua mbalimbali ambazo Serikali imekuwa inaendelea kuzifanya kuboresha ili dhana nzima ya haki jinai na pia nimeeleza katika Bunge lako kwamba katika moja ya hatua kubwa ambayo imefanyika ni mashirikiano na taasisi mbalimbali zisizo za Kiserikali, Asasi za Kiraia na Taasisi za Dini na Vyuo vinavyotoa elimu ya sheria juu ya andiko lililotolewa kutafuta maoni ya watalaaam hawa ili tuweze kufikia sehemu ya kujadili mambo yote ya msingi yanayoambatana na issue za haki jinai.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:**  
Mheshimiwa Spika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na sheria zetu zipo wazi kabisa juu ya masuala ya haki jinai na katika eneo hilo la haki jinai ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tuna pande mbili kuna wanaotenda jinai na wanaotendewa jinai. Sasa kama mpango mzima utakuwa ni kuwatetea walioienda jinai uelewe upande wa pili kuna walioienda jinai. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tulikuwa tuna tatizo la panya road, sasa inasemwa hapa kama vile polisi wasikamate mpaka upelelezi upatikane na ndiyo maana tulipotunga hii sheria mwaka huu nafikiri tuliweka wazi kwamba kwa baadhi ya makosa ya kawaada ambayo hauoni sababu ya haraka ya kwenda kumkamata mtu kama upelelezi haujakamilika tunaweza tukasema yawe hivyo, lakini kwa kweli ni lazima tujue kwamba watu wanaotendewa makosa ndiyo wanaotakiwa kuonewa huruma zaidi na kusaidiwa kuliko wanaotenda makosa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niombe rai kwamba twende hivyo kwasababu kwa kufanya hivyo ndiyo maana nchi ipo salama hata leo hii.

Vinginevyo tukibadilisha jurisprudence hapa tunaweza tukaharibu kabisa haki jinai ikawa ni tatizo, lakini haki jinai inapande mbili. Ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa ajili tu yakuliweka sawa wale wanaokuwa huko watafikia hicho kitendo cha kuitwa wametenda jinai baada ya Mahakama kuwa imetoa uamuzi. Kwa hiyo, ni pande mbili kwa maana ya watuhumiwa wa kutenda jinai na wale waliotendewa jinai.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri ameshajibu maswali ya kutosha hapa, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. (Makofii)

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 140

### **Mpango wa kukuza uchumi wa buluu**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhusu mpango wa kukuza uchumi wa buluu kwa kuzingatia mazao yatokanayo na bahari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Engineer Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukuza uchumi wa buluu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi chini ya uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais na kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo, mashirika ya kijamii, na sekta binafsi tunaandaa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Buluu. Mazao ambayo yamepewa kipaumbele kwenye mkakati huo kwa upande wa baharini ni samaki aina ya dagaa, pweza, kambamiti, vibua, jodari, changudoa, zao la mwani, unenepeshaji wa kaa na ukuzaji wa lulu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 11.51 ambazo zitatumika kununua boti za kisasa zenye engine, kifaa cha kutafutia samaki (GPS) na kasha la ubaridi lenye uwezo wa kubeba tani 1.5 kwa ajili ya kuwakopesha wavuvi. Pia jumla

ya shilingi bilioni 20 zimetengwa ambapo kiasi cha shilingi bilioni 3.32 zitatumika kuwezesha pembejeo kwa ajili ya wakulima wa mwani katika ukanda wa bahari ya Hindi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri huyo anaitwa dhangudoa au changu mwenye madoa? (Kicheko)

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, samaki huyu ana aina mbili, tatu katika mpango mkakati yupo changu na yupo changudoa. Changudoa ndiyo tumemkusudia katika mkakati wetu si changu wa kawaida. (Kicheko)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kama ndivyo hilo linakuwa ni neno moja au ni maneno mawili tofauti yaani changu halafu doa ili Kiswahili, kwa sababu tunataka Kiswahili chetu kikae sawasawa.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nadhani hili ni jina na jina linategemeana na mtamkaji wa lile jina.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'azi Ullenge, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoa na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwani limekuwa ni zao ambalo linaingizia nchi nyingi fedha za kigeni na uzalishaji Tanzania kwa sasa ni tani 3,500 tu, lakini uhitaji uliopo kwa wanaotu-approach nchini kwetu ni tani zisizopungua 10,000. Swali langu ni kwamba ni upi mkakati wa Serikali wa kuongeza uzalishaji wa mwani nchini? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kutoka Tanga, ukanda huu wa mwambao wa bahari ya Hindi mpaka Mtwara, zaidi ya kilometra 1,084 kuna vikundi vya wanawake visivyopungua 8,000. Naomba kujua ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha masoko kwa wanawake hawa wanaozalisha mwani nchini na bei yenye tija?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa, Engineer Mwanaisha Ng'azi Ulunge, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, la kwanza katika jibu la msingi nimeeleza juu ya mkakati wa Serikali wa kuweka shilingi bilioni 3.3 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakopesha vikundi vya akina mama kamba na kitu tunaita taitai, na kitu tunaita mbegu ili waweze kuongeza uzalishaji. Na hiyo tutagawa katika vikundi vyote pamoja na hivi vikundi alivyovitaja Mheshimiwa Ulenge. Kwa hiyo, hilo litasababisha kuongezeka kwa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, suala la bei na soko, nataka niwahakikishie kwamba kwa hali ilivyo na kwa uelekeo tunaouona, soko la mwani linazidi kukua siku hata siku na kwa msingi huo, tutakapokuwa na uzalishaji mkubwa, sasa uwezo wa kuweza kuliongoza soko katika bei utakuwa ni mkubwa, ni pamoja na kuweka mkakati wa bei elekezi ili zisishuke.

Mheshimiwa Spika, kama mwani aina ya spinosio uuzwe 800 kwenda juu, kama mwani wa aina ya kotonii uuzwe 2,000 kwenda juu. Huo ndiyo mkakati wetu tunaouelekea. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, sasa aulize swali lake.

Mheshimiwa Mtaturu huko umeme umekatika? Haya ahsante sana.

Na. 141

### **Huduma ya Treni Manyoni – Singida**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itarudisha huduma ya treni Manyoni – Singida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TRC katika bajeti ya mwaka 2022/2023 imetenga fedha kwa ajili ya kufanya tathmini na maadalizi ya awali ya kufufua njia ya Manyoni – Singida yenye urefu wa kilometra 115 ambayo ilifungwa takribani miaka 30 iliyopita. Lengo la kufufua njia hii ni

kuboresha usafirishaji wa mizigo na abiria pamoja na kukuza uchumi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) inaendelea na mchakato wa ununuzi wa wakandarasi watakaofanya tathmini ya mahitaji na maandalizi ya awali ya kutekeleza mradi huo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo yanaleta matumaini kwa wananchi wa Singida kwa kufufua reli hii ya Singida – Manyoni. Pamoja na majibu hayo, ninayo maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kupata *commitment* ya Serikali, nataka kujua ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa lengo la reli hii lilikuwa ni kukuza uchumi, kubeba mizigo ambayo ipo katika ukanda huu na hasa ililenga sana wakati huo Mwalimu Nyerere akianzisha reli hii ni kubeba ngano ambayo iko kule Basutu katika Mkoa wa Manyara. Sasa kwa sababu tunakuza eneo la kilimo na tuna madini yako pale kwenye Mkoa wa Singida, ni mpango gani wa Serikali sasa kuujenga kwa kiwango cha SGR ili iwe na uwezo mkubwa wa kubeba mizigo katika eneo hilo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Singida Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2022/2023, tumetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 3.45 kwa ajili ya ukarabati wa tuta pamoja na makalavati na uwekaji wa tabaka la kokoto na tutajenga kama ambavyo tuliboresha reli ya kutoka Tanga kwenda Arusha kupitia Moshi kwa maana ya kutumia *force account*.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, anapenda kujua ni lini sasa hii reli itakuwa katika kiwango cha *standard gauge*? Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa jitihada zake pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wa Mkoa wa Singida, Serikali mara baada ya kufanya ukarabati huu wa awali, tukifungua malango/tukifungua njia, ndipo tutakapoanza sasa kufanya tathmini, *feasibility study* kwa ajili ya SGR. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, naona umesimama, swali linahusu kurudisha huduma ya treni Manyoni na Singida, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, ni lini treni ya mwendokasi itaanza kufanya kazi kati ya Dar es Salaam na Morogoro? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Morogoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matarajio yetu yalikuwa reli ya SGR kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro yenyeye urefu wa kilometra 300 tulitegemea ingeanza mwezi huu wa Septemba kama ambavyo tulijibu hapo awali wakati wa Bunge la Bajeti. Lakini kutohana na changamoto mbalimbali hususan katika kusafirisha vipuri na mabehewa ambayo kulikuwa kuna changamoto ya kupata meli ya usafirishaji kutoka nchini Ujerumani kuja Tanzania, lakini habari njema kwa Watanzania wote watambue ya kwamba tayari vichwa vyta treni, mabehewa ya abiria na mizigo, hivi ninavyosema vimekwishapakiwa kwenye meli kuja nchini Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunataraji kwamba ifikapo mwezi Novemba, mwaka huu vitakuwa vimeshaingia na tutafanya majaribio mpaka mwezi Januari. Kwa hiyo, mwezi Februari mwakani standard gauge kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro itaanza rasmi, ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nafurahi kwamba umetaja miezi ambayo sisi wenyewe tutakuwepo hapa Dodoma, kwa hiyo tutakuwa washuhudiaji wa jambo hilo. Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge wa Ukonga, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula.

Na. 142

### **Ujenzi wa Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Dar Es Salaam**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA K.n.y. MHE. JERRY W. SILAA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Pugu – Kifuru hadi Mbezi Mwisho kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge wa Jimbo la Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho yenye urefu wa kilometa 12.7, sehemu ya kutoka Mbezi Mwisho hadi Kifuru (kilometra 6.7) imejengwa lami kwa njia mbili na sehemu ya kutoka Kifuru – Pugu Station (kilometra 6) ni barabara ya vumbi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kazi ya upembusi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu ya Pugu Station hadi Kifuru (kilometra sita) kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa njia nne na kwa sehemu ya Kifuru – Mbezi Mwisho (kilometra 6.7) kuipanua kutoka njia mbili kuwa njia nne. Zabuni kwa ajili ya kumpata mhandisi mshauri wa kufanya kazi hiyo zimetangazwa na zitafunguliwa tarehe 10 Oktoba, 2022. Baada ya kazi ya usanifu kukamilika Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, na ni matarajio ya wananchi wa Jimbo la Ukonga ya kwamba barabara hizi zitatekelezwa kwa wakati kama Serikali ilivyoagiza.

Mheshimiwa Spika, swali dogo la nyongeza; kwa kuwa Serikali inao mpango na barabara nyingi zimeahidiwa ikiwemo barabara ya Msongola – Mbande yenye jumla ya kilometra 4.95. Ni lini Serikali inatoa ahadi ya kuanza kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kwa niaba ya Mheshimiwa Jerry Silaa wa Ukonga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara ya Msongola – Mbande hadi Mbagala (kilometra tano) sisi tunasema bado hazijajengwa kwa kiwango cha lami. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeanza mpango

na tayari zabuni zimeshatangazwa. Tutaanza kujenga kilometra mbili kwa mwaka huu wa fedha, ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Manase Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. na mimi ninapenda kujua ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mbalizi – Shigamba ambayo ni kiungo cha mikoa ya Mbeya na Songwe kupitia lleje, na pia ni kiungo kwenda Nchi jirani ya Zambia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijiji, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbalizi – Shigamba tayari zabuni zinaandaliwa kuitangaza kwa ajili ya kufanya feasibility study na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi kwa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo mwaka huu tutahakikisha tunakamilisha feasibility study pamoja na usanifu wa kina, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zueno Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mwembe – Mbaga – Mamba ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Hayati Rais Dkt. Magufuli?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mwembe – Mbaga ambayo iko Same ni barabara ambayo iko kwenye miinuko. Tulichokifanya kwa sasa, kabla ya kuanza kujenga kwa kiwango cha lami ni kuainisha maeneo yote korofii na yenye miinuko ili tuweze kuyadhibiti na yaweze kupitika kwa mwaka wote, na baada ya hapo Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kufanya feasibility study na usanifu wa kina ili kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Murushaka kwenda mpaka Murongo, ahadi ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, kilometra 50, imeshatangazwa muda mrefu lakini mpaka sasa hivi haijaanza ujenzi; nini tatizo lake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara haina shida, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tulishatangaza, mzabuni (mkandarasi) alishapatikana na tunategemea muda wowote ataoneshwa site ili aanze kutekeleza hiyo kazi, kilometra 50, kama zilivyoahidiwa na kama tunavyotegemea mkandarasi aanze kuifanya hiyo kazi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dodoma ni jiji kama yalivyo majiji mengine na hivyo linapaswa kuwa na hadhi zote za jiji. Sasa swali langu; ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara za mitaani kwa kiwango cha lami kwa mitaa yote ya Jiji hili la Dodoma?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa TAMISEMI, sijui yuko hapa? Ama Waziri wa TAMISEMI. Haya, Serikali ni moja, lakini barabara za mitaa ziko TARURA ambayo ni TAMISEMI; Mheshimiwa Naibu Waziri, wasaidie TAMISEMI kujibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lambert kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie kwamba jitihada kubwa sana zinafanyika kufanya kwamba barabara zote za Jiji la Dodoma zinafanyika. Tuna barabara za *outer ring circuit* na za *inner ring circuit*, lakini pia barabara zote ziko kwenye mpango kuhakikisha kwamba zinapanuliwa na kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuhakikisha kwamba jiji linakuwa kweli na hadhi ya jiji, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Ni lini Serikali itaimarisha, kuboresha na kudhibiti korongo kwenye Mlima wa Mawono, barabara ya Unyoni kuelekea Maguu wakati tunasubiri utekelezaji wa ujenzi wa lami kama Serikali ilivyoahidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mbunge wa Mbanga Vijiijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, korongo alilolisema naomba nitumie nafasi hii kumuagiza Meneja wa Mkoa wa Ruvuma aende akalitathmini na aone kazi ilivyo ili tuweze kupata ghamama na tuweze kulikarabati ili isije ikaleta madhara ya kukata mawasiliano ili tuweze kulikarabati kabla ya kuanza kujenga hiyo barabara ama kuifanyia usanifu kwa maandalizi ya kujenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana; Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nina swali dogo la nyongeza kuhusiana na barabara inayotoka Mbagala kuelekea Temeke kutokea Kilungule - Mbagala kuititia Buza Kwa Mpalange; ni lini sasa itakamilisha ile lami? Kwa sababu wananchi wanapiga kelele sana. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dorothy Kilave, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara zetu nyingi za TANROADS na TARURA zinaingiliana. Lakini nitumie tu nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba azma ya Serikali ni kuzijenga barabara zote kwa kiwango cha lami na kwa kuwa barabara zimeshaanza kujengwa, tunamhakikishia kwamba Serikali itazikamilisha hizo barabara, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mlowo – Kamsamba kupitia Utambalila na Chitete ikiwa iko kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2025? Ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mbunge wa Mombasa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara Kamsamba – Utambalila – Chitete ni barabara ambayo ni sehemu ya barabara ya Mlowo – Utambalila – Kamsamba; barabara hizi ziko kwenye package moja. Kwa sababu tulishakamilisha usanifu, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kujenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunionna.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Buguni kuanzia Tengeru sokoni kupitia Kikwe hadi Mererani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ni barabara ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa eneo hilo na Serikali ina mpango wa kujenga kwa kiwango cha lami. Ikiishakamilisha usanifu wa kina barabara hii tutajenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu sasa aulize swali lake.

### **Usajili wa Wakulima Nchini**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha usajili wa wakulima wote nchini hasa wa mazao ya kimkakati ikiwemo pamba, korosho, kahawa, chai na michikichi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikisajili wakulima kupitia mifumo mbalimbali ikiwemo Bodi za Mazao, Sensa ya Kilimo na Vyama vya Ushirika. Hadi Agosti, 2022 jumla ya wakulima 1,499,989 wa mazao ya kimkakati ya chai wakulima 31,093, pamba wakulima 556,384, kahawa 305,261, korosho 483,034, miwa 6,746, mkonge 2,369, pareto 10,846, tumbaku 53,758 na mazao mengine 50,498, wamesajiliwa kwenye Mfumo wa Usajili wa Wakulima (*Farmers Registration System*) na vyama vitatu vya ushirika wa michikichi wamesajiliwa. Serikali imeanza kupitia upya mifumo ya usajili wa wakulima kwa lengo la kuwa na mfumo mmoja utakaowezesha usajili wa wakulima wa mazao yote nchini ili kurahisisha upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani na masoko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, hizi zimekuwa ni namba tu ambazo zikisomwa kila mwaka; lakini ukienda kwenye uhalsia kabisa huwezi kukuta mkulima mfano wa pamba ana kitambulisho cha usajili, hata kwenye korosho huwezi kukuta mkulima kwenye korosho ana kitambulisho cha usajili. Ukiangalia hata Chama chetu cha Mapinduzi juzi tu kimesajili wanachama wake, lakini tayari wamepewa kadi.

Sasa mimi nataka njue kauli ya Serikali ni lini sasa hawa wakulima wa mazao ya kimkakati watapewa kadi za usajili ambazo zitakuwa kama vitambulisho kwao?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; tumekuwa zikiagizwa pembejeo nyingi ambazo zinakuja kwa wakulima lakini madhara yake zinakuwa zinabaki kwa sababu uhalsia kamili wa wakulima waliosajiliwa bado haujajulikana. Nataka nipate majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu kama ifuatavyo na nitayajibu kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali tunaendelea na zoezi la usajili wa wakulima nchi nzima ambapo mfumo unaotumika hivi sasa ni mfumo ambao unampa kila mkulima utambulisho maalum kwa maana atakakuwa na namba yake maalum ambayo ndiyo utakuwa utambuzi wake. Zoezi hili linaendelea katika maeneo mengi kwa ukamilifu mzuri na uratibu unaendelea vizuri na tunaamini kabisa likikamilika litatibu changamoto zote ambazo wakulima wanazipata hasa katika utambuzi wao kwa sababu kila mkulima atapata namba yake maalum ya utambuzi; na tunaamini kupitia hapo sasa hata zile huduma muhimu watazipata kwa rahisi zaidi.

Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hili linaendelea na linaendelea vizuri na mwisho wa siku tutakuwa na kanzidata ya wakulima wote nchini kila mtu kwa maeneo yake alipo pamoja na maeneo ambayo anayamiliki na mazao anayalima na yields anazipata.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 144

### **Ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji Muleba**

**MHE. DKT.OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa skimu za umwagiliaji Wilayani Muleba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Kamati Shirikishi ya Umwagiliaji Mkoa na Ofisi ya Kilimo Wilaya ya Muleba imekamilisha tathmini ya kina ya mahitaji ya sasa ya skimu za umwagiliaji za Buyaga hekta 120, Kyamyorwa hekta 500, Kyota hekta 120 na Buhangaza hekta 600 na kupata gharama halisi za umaliziaji wa ujenzi wa skimu hizo. Serikali inaendelea na

zoezi la kuainisha maeneo mengine yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji Wilayani Muleba likiwemo Bonde la Buligi lenye takribani hekta 5,000.

Mheshimiwa Spika, skimu hizo zitaingizwa katika mpango wa ujenzi na ukamilishaji wa skimu za umwagiliaji katika kipindi cha mwaka 2023/2024 na 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipatia fursa ya kuuliza maswali mawili madogo nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hizi Skimu za Buhangaza, Kyota na Kyamyorwa ni za muda mrefu, zilijengwa kwa fedha za walipa kodi wa Tanzania lakini hazijakamilika kwa maana hiyo tumezamisha fedha za walipa kodi lakini hakuna tunachokipata.

Je, hizi skimu nataka kupata *commitment* ya Serikali ni lini zitakamilishwa ili ziweze kutumika kama ilivyokusudiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kagera tumebarikiwa kuwa na bonde Mto Ngonon, ni bonde kubwa linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanza kulitumia hilo Bonde la Mto Ngonon kwa kilimo cha umwagiliaji? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya msingi nimeeleza mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwanza tumeefanya tathmini ya kina ya skimu hizi kufahamu gharama halisi na baadaye utekelezaji wake utaanzia mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili la kuhusiana na Bonde la Mto Ngonon, niliwalii kutoa maelezo hapa naomba niyarudie; ukiangalia katika jedwali la saba katika kitabu cha bajeti cha Wizara ya Kilimo tumeainisha mabonde 22 ambayo Serikali itakwenda kuyapitia kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina likiwemo Bonde la Mto Ngonon.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaondoe hofu Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Mkoa wa Kagera nafahamu hili ni eneo ambalo mmekuwa mkilipa kipaumbele kikubwa sana, tumeanza na upembuzi yakinifu tutajenga

skimu katika Mto Ngono na umwagiliaji utafanyika na wananchi wa Kagera watanufaika na bonde hilo. (Makofi)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe sasa aulize swali lake.

Na. 145

**Vivutio vya Utalii Viliviyotambuliwa – Ukerewe**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, ni vivutio gani vya utalii vimetambuliwa Wilayani Ukerewe na hatua zippi zimechukuliwa kuendeleza na kuvitangaza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara katika kipindi cha mwaka 2020/2021 kwa kushirikiana na maafisa wa Mkoa wa Mwanza walitekeleza zoezi la kubaini na kuvitambua vivutio vya utalii vilivyopo katika Kisiwa cha Ukerewe. Vivutio hivyo ni pamoja na utalii wa ikolojia, utalii wa fukwe, utalii wa kiutamaduni na kihistoria.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mikakati ya kuvitangaza na kuviendeleza vivutio hivyo vya utalii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa utalii hapa nchini. Sambamba na hilo Serikali inaendelea kuimarisha Ofisi ya Kanda ya Utalii iliyopo Jiji la Mwanza na kuanzisha Chuo cha Utalii cha Taifa katika Mkoa wa Mwanza kwa lengo la kusogea huduma za Kanda ya Ziwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Nitambue kazi kubwa inayofanywa na Wizara hii, pamoja na kutambua mikakati hii ambayo itasaidia kutangaza

na kuviendeleza lakini bado sisi tulioko kwenye maeneo yale ikiwa ni pamoja na wataalam wa halmashauri hawana uelewa wa mikakati hii.

Sasa Mheshimiwa Waziri yupo tayari baada ya Bunge hili kuja Ukerewe ili kwa pamoja sasa wao na sisi pamoja na wataalam wa halmashauri tuweze kushirikishana mikakati hii ili iweze kuwa na tija?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; moja kati ya vivutio vilivyoko Ukerewe ni pamoja na beach ya Rubya ambapo pia kuna msitu ulio chini ya TFS. Lakini kwa kuwa Ukerewe tuna upungufu wa madawati karibu 6,000; Mheshimiwa Waziri kupitia CSR, TFS wako tayari kutusaidia kuondoa upungufu huo wa madawati 6,000? Nashukuru. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niko tayari kuambatana na Mbunge kwenda katika Kisiwa cha Ukerewe kuibua vivutio vilivyopo, lakini pia kuvitangaza. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lakini suala hili la pili la kuhusu beach ya Rubya ni kweli tuna hifadhi ya Rubya ambayo ni hifadhi ya msitu unaosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania na tumekuwa tukitoa CSR katika maeneo hayo na hivi karibuni tunakwenda kuzindua Kituo cha Polisi ambacho kimejengwa kutohana na hii Hifadhi ya Rubya. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba wajibu wa Serikali ni kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo tunayahifadhi wananchi walioko kwenye maeneo hayo wanafaidika na rasilimali iliyoko pale. Kwa hiyo, suala la madawati tutakwenda kulishughulikia na tutakwenda kuzungumza na wananchi ili waone umuhimu wa kuendeleza hifadhi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali sasa aulize swalii lake.

Na. 146

#### **Kuboresha Hifadhi ya Taifa Kitulo**

**MHE. FRANCIS L. MTEGA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuboresha Hifadhi ya Taifa Kitulo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa Kitulo ni hifadhi ya kipekee ambayo huwezi kuifanananisha na hifadhi nyingine hapa nchini. Hifadhi hii ina utalii wa maua, maporomoko ya maji, ndege wa aina mbalimbali na vivutio vingine. Wizara kwa kutambua hilo imeendelea kuboresha miundombinu ndani ya hifadhi. Miundombinu hiyo ni pamoja na kuimarisha barabara zilizomo ndani ya hifadhi, kuanzisha huduma za malazi na chakula, kuongeza mazao mapya ya utalii ndani ya hifadhi kama vile utalii wa kutumia baiskeli, utalii wa kutembea kwa miguu na utalii wa kupanda vilima.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo ndani ya hifadhi hiyo ikiwemo maeneo ya malazi na shughuli za utalii kama vile utalii wa farasi, utalii wa kubembea na kamba na mazao mengine ya utalii ili kuongeza idadi ya watalii na idadi ya siku za kukaa hifadhini na hivyo kuongeza mapato zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, nakushuruku sana lakini pia nashukuru sana majibu mazuri ya Serikali, hata hivyo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, kutoka barabara kuu kufika Kitulo pana mlima wenye kona 54 na nyani wa kutosha. Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara ile kwa kiwango cha lami ili watalii wakafurahie nature ya uumbaji wa Mwenyezi Mungu? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pili; je, Wizara ina mpango gani wa kujenga ofisi walau ndogo pale Chimala ili kuamsha ari ya wananchi pale kujenga mahoteli ya kitalii jambo ambalo litaleta fursa ya ajira kwa vijana na kuinua uchumi wa Wanambarali? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbalali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna changamoto ya barabara hii na tutazungumza na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi ili tuone namna ya kujenga

barabara hii kwa kiwango cha lami na hii itasaidia kuvutia utalii katika maeneo yanayozunguka Hifadhi ya Kitulo.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala hili la ujenzi wa ofisi ninaomba nilichukue tukafanye tathmini kuangalia namna iliyo bora ya kufikika kiurahisi, lakini pia kuwepo na hicho kituo ambacho kinawezesha muendelezo wa utalii. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali fupi la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA,** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kuna mpango gani wa kuboresha miundombinu ya Hifadhi za Ibanda na Rumanyika zilizopo Wilaya ya Kyerwa ili kuvutia watalii? (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna hifadhi nyingi ambazo tumeshazitangaza ikiwemo ya Ibanda, Rumanyika, pia Kyerwa. Nimuhidi tu Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa Mkakati wa Serikali ni kuhakikisha tuna zindua Phase II ya programu ya Royal Tour. Kwa hiyo, maeneo haya pia tutaweza kuyaingiza ili yaweze kuwa ni ya kimkakati katika kuhakikisha kwamba vivutio hivi tunavitangaza vizuri. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Muhamrami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo sasa aulizwe swali lake.

Na. 147

### **Hitaji la eneo la makazi kwa wananchi wa Kata ya Makurunge**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, ni lini wananchi wa Kata ya Makurunge watapatiwa eneo la makazi la Razaba baada ya maeneo yao kuchukuliwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali namba 147 la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati eneo hili linachukuliwa na Serikali kwa ajili ya uwekezaji wananchi waliokuwa wakazi wa eneo hilo walilipwa fidia stahiki kwa mujibu wa sheria. Aidha, tunatambua uwepo wa wananchi 16 ambaa wamekuwa wakidai kulipwa fidia zao, Serikali inaendelea kushughulikia madai hayo na yatakapokuwa tayari tutawapa taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inadaiwa viwanja takribani 1,000 na pia hao wananchi wa Makurunge hawana sehemu ya kukaa ambayo ipo sahihi.

Je, ni lini Serikali au Wizara itawapatia Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo mashamba mawili ambayo ni Greenwood na Jeneta ambayo umiliki wake ni wa utata ili kuweza kuwasidia wananchi hawa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Waziri ni lini anaweza akaja Bagamoyo ili kuja kuyaangalia yale mashamba ya Greenwood na Jeneta ili atoe tamko la Serikali kuhusu umiliki wake yale mashamba? (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, juu ya shamba la Greenwood na Jeneta nadhani taratibu za kisheria zinazeleza na wananchi wa Bagamoyo wanatakiwa wafuate hizo taratibu kama kutakuwa na ulazima wa kufanya hivyo ili kama Serikali itajiridhisha juu ya maombi yao na kama ninavyosema kwamba kutakuwa na utata wowote basi tutaangalia kuona jinsi gani tunaweza kuliamua.

Mheshimiwa Spika, juu ya suala la pili, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie tutakamaliza Bunge hili katika kipindi nitakachokwuwa kwenye

ziara katika Jimbo langu litakuja Bagamoyo ili tuweze kushughulikia kero hiyo.  
(Makof)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Flatey Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijiji sasa aulize swali lake.

Na. 148

### **Ujenzi wa minara ya mawasiliano – Mbulu**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, lini minara ya mawasiliano itajengwa katika Kata za Endanywish, Endagulda, Gidurdagaw, Yaeda Ampa, Hayeda na Endanilay?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Nape Moses Nnauye majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kkuna mnara umejengwa katika kata ya Bashay kijiji cha Bashay kwa lengo la kutoa huduma katika kijiji cha Bashay na baadhi ya maeneo ya Yaeda Ampa. Hata hivyo, baada ya ujenzi wa mnara kukamilika, bado ilionekana kuwa Vijiji vya Arri na Hayeseng kutoka Kata ya Yaeda Ampa bado havipati huduma nzuri ya mawasiliano na hivyo vililingizwa katika orodha ya miradi ya Tanzania ya Kidigitali ambapo zabuni ya mradi huu inatarajiwa kutangazwa hivi karibuni mara idhini ya benki itakapotolewa.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Serikali kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imeziingiza Kata za Endahagichan yeye Vijiji vya Endadubu, Miqaw na Endahagichan, Kata ya Eshkesh yeye Vijiji vya Domanga na Endagulda, kata ya Geterer yeye Vijiji vya Magong na Mewada, Kata ya Haydarer yeye Kijiji cha Gidbiyo, Kata ya Masqaroda yeye Kijiji cha Harbanghet, na Kata ya Yaeda Chini yeye Kijiji cha Endajachi katika mradi wa Tanzania ya Kidijitali ambao kama nilivyosema zabuni yake inatarajiwa kutangazwa hivi karibuni. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kata za Endanywish, Endagulda, Gidurgadaw, Hayeda na Endanilay tathmini ilifanyika na maeneo hayo

yalionekana yana changamoto za upatikanaji wa huduma za mawasiliano na hivyo yataingizwa katika orodha ya miradi ambayo zabuni yake itatangazwa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. (Makof)

**SPIKA:** Mheshimiwa Platei Massay swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante nampongeza kwanza Mheshimiwa Waziri kwa kusoma vizuri vijiji hivyo, lakini kuna mnara ambao uko Masqaroda haujawaka mpaka leo na umejengwa kwa gharama kubwa.

Je, lini Mheshimiwa Waziri mnara huu utapata kuwaka ili mawasiliano yakapatikana Jimbo la Mbulu Vijiji?

Pamoja na majibu yako haya na kata ulizotaja na kwa kuwa hakuna uhalisia wa kutosha; je, uko tayari kufuatana na mimi kwenda Jimboni ukayaona haya yote uliyoyasema na majibu yako haya? (Makof)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Massay Mbunge wa Mbulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mnara alioutaja umejengwa na umekamilika kwa maana ya vifaa, lakini ulikuwa haujawashwa kwa sababu tulikuwa na changamoto ya vifaa vya mwisho vya kuwashia ule mnara kutokana na tatizo la covid uzalishaji wa baadhi ya vifaa ulichelewa, lakini sasa vifaa viro tayari na mnara huu utakwenda kuwashwa.

Mheshimiwa Spika, pia niko tayari kuambatana naye tumekuwa tukishirikiana naye katika kutatua tatizo la mawasiliano katika eneo lake; na yeye anajua kwamba hata katika mradi wa kidijitali tumeweka zaidi ya minara saba kwenye Jimbo lake kwa ajili ya ku-facilitate mawasiliano. (Makof)

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali fupi la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi. Kijiji cha Uliwa kata ya Uhungilo kijiji ambacho kina shule, kina sekondari, kina zahanati lakini hakina mawasiliano kabisa ya aina yoyote, ni lini sasa Serikali itapeleka mawasiliano katika kijiji hicho cha Uliwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**23 SEPTEMBA, 2022**

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Mwanyika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli maeneo aliyoyataja ni katika orodha tuliowasilisha hapa Bungeni katika ile miradi 763 ya Tanzania ya kidijitali, maeneo aliyoyataja baadhi yake yamo na nimuhidi kwamba tutakapotangaza miradi hiyo basi ujenzi utaanza mara moja. (Makof)

**SPIKA:** Kuna swali lingine Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Ranya sasa aulize swali lake.

Na. 149

### **Hitaji la Mawasiliano katika Kata za Mpakani mwa Tanzania na Kenya**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano katika Kata za Ikoma, Roche, Gobire na Bukura zilizopo mpakani mwa Tanzania na Kenya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Ranya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Bukura Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umeingia makubaliano na Kampuni ya Simu ya Halotel tarehe 30 Agosti, 2022 kwa ajili ya ujenzi wa mnara katika Kijiji cha Kirongwe kilichopo katika Kata ya Bukura. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa Kata za Ikoma na Roche zilizopo katika Jimbo la Ranya zimejumlishwa katika kata 763 ambazo zabuni ya kata hizo kwa ajili ya kupeleka huduma za mawasiliano inatarajiwa kutangazwa mapema mwezi Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kata ya Gobiro, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umepokea changamoto hiyo na kwamba eneo husika litafanyiwa tathimini na litaingizwa kwenye zabuni za miradi ya mawasiliano itakayotangazwa kwa mwaka wa fedha 2023/ 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kata ya Roche pamoja na Ikoma kujumuishwa katika Kata 763 ambazo utekelezaji wake kwa maana ya zabuni kutangazwa mwezi Oktoba, lakini kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa sana wa ujenzi wa minara maeneo mengi nchini hata pale panapokuwa no objection imetoka, lakini bado ujenzi wa minara mingi nchini unakuwa umechelewa.

Nilitaka nipate kauli ya Serikali juu ya hili kwamba ni nini kinasababisha pamoja na kwamba no objection inakuwa imetoka lakini ujenzi wa minara inachukua miaka miwili mpaka mitatu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ni mara ya tatu nauliza swali hili Kata ya Bukura, Kata ya Ikoma, Goribe pamoja na Roche ni kata ambazo ziko mpakani, lakini haziwasiliani hakuna mawasiliano ya Kitanzania.

Nilitaka nijue kwa sababu hiyo ya kukosa mapato pamoja na usalama wa Kata zile nini kauli ya Serikali juu ya ujenzi na utekelezaji wa minara maeneo ya mpakani kwa dharura na kwa haraka ili kusaidia maeneo yale ya kimpakani ndani ya nchi yetu? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chege, Mbunge wa Rarya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni kweli kwamba imekuwa inatuchukua miezi tisa mpaka 12 kujenga mnara ambayo ndio ilikuwa hali iliyokuwa imezoleka na sababu yake ni moja tulikuwa tunatumia miezi sita kutafuta vibali mbalimbali vya kujenga hiyo minara kwenye maeneo husika, lakini tunashukuru Wizara ya Mazingira chini ya kaka yangu Mheshimiwa Jafo sasa wamerahisisha badala ya kutumia kwa miezi sita tumeweza baadhi ya maeneo ikiwemo Zanzibar kupata vibali ambavyo tulikuwa tunatumia miezi sita tumepata kwa mwezi mmoja na hivyo muda wa kujenga minara umepungua sana. Uzoefu uliotokea Zanzibar tumejenga kwa siku 90 kwa hiyo, tunaamini hata eneo hili tutakapopata no objection mradi huu utachukua miezi isiyozidi minne na tuna hakika kwamba utakuwa umekamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kata husika alizositaja ni kweli ziko mpakani na yeye na Mkuu wake wa Wilaya wamekuwa wakiwasiliana na sisi mara kwa mara. Changamoto iliyotupata ni kwamba tulipotangaza tender ya kujenga minara kwenye maeneo haya, hawakupatikana wajenzi tukarudia kutangaza mara ya pili na bado mkandarasi hakupatikana.

Tulichoamua tumeamua kuchukua miradi kwenye kata hizi na kuingiza kwenye Tanzania ya Kidigitali ambayo package yake kidogo ni nzuri. Kwa hiyo, wakandarasi watapatikana, nimtoe shaka nia yetu ni kuhakikisha maeneo ya mipakani inapata mawasiliano ya kutosha na hasa kwa sababu biashara ya mpakani ni kubwa na sisi tunapenda kufanya biashara kwenye maeneo hayo. Nimhakikishie kwamba minara hii itajengwa na itajengwa kwa wakati. (Makofij)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Festo Richard Sanga Mbunge wa Makete swali litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Neema Mgaya.

Na. 150

#### **Ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mto Lumakali – Makete**

**MHE. NEEMA W. MGAYA K.ny. MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mto Lumakali Wilayani Makete?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Steven Rujwahuka majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TANESCO inaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Rumakali wa kuzalisha megawati 222 ulioko katika Wilaya ya Makete, Mkoani Njombe.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2022/2023 Serikali imetenga shilingi bilioni nane kwa ajili ya maandalizi ya awali ya mradi wa Rumakali. TANESCO imehuisha upembuzi yakinifu pamoja na kukamilisha nyaraka za zabuni za kumpata mkandarasi wa ujenzi. Aidha, uthamini wa mali za wananchi zinazopitiwa na mradi utakamilika mwezi Oktoba, 2022. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwaka ujao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Mimi na Mheshimiwa Festo Sanga tunaishukuru Serikali kwa hatua za

awali kuhusiana na bwawa hili, lakini tulikuwa tunataka Serikali ituhakikishie ni lini wananchi wetu watalipwa fidia?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Makete wamekuwa na changamoto kubwa sana ya kukatika katika kwa umeme kwa muda mrefu kwa sababu umeme huo unatoka Mbeya.

Je, Serikali inawahakikishia nini wananchi wa Makete kwamba bwawa hili litakuja kuwa tija ya kutatua changamoto hiyo? (Makofij)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Neema Mgaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la kwanza baada ya kukamilisha uthamini mwezi Oktoba ndiyo sasa taratibu za malipo zitaanza ikiwa ni kupelekea Mthamini Mkuu wa Serikali na fedha tayari imeshatengwa. Kwa hiyo, baada ya kukamilisha taratibu hizo fedha italipwa, tunaamini kabla ya kufikia mwanzoni mwa mwaka unaokuja wa fedha taratibu zikienda kama zilivyopanga fedha za fidia zitakuwa zinalipwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili ni kweli mradi huu ukikamilika utawafaa wananchi wa Mkoa wa Njombe, Wilaya ya Makete, lakini na Watanzania wengine wote kwa sababu ni mradi utakaopeleka umeme kwenye Gridi ya Taifa. Katika kipindi hiki ambacho umeme unakatika katika Serikali imeshafanya tathimini ya kujenga vituo vingine vya kupoza umeme kwenye maeneo mbalimbali na Makete ni eneo mojawapo ambalo limetizamwa kwa ajili ya kuboresha huduma ya umeme.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, sasa aulize swali lake.

Na. 151

#### **Uwekezaji wa Miradi 294**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha uwekezaji wa miradi 294 yenye thamani ya dola bilioni 8.04 inatekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Jimbo la Lulindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa uwekezaji wa miradi 294 yenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 8.04 inatekelezwa, Serikali imeendelea kufanya ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa mazingira ya uwekezaji nchini yanaendelea kuboreshwa ili kurahisisha utekelezaji na kuvutia mitaji zaidi. Aidha, kuimarisha Kituo cha Huduma ya Mahala pamoja, kutoa huduma za mahala pamoja kwa njia ya kieletroniki lakini pia kuendelea kuwashudumia wawekezaji baada ya kukamilisha uwekezaji. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mchungahela swalii la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni miradi mingapi ya uwekezaji kati ya hiyo 294 imeanza?

Lakini pili, je, Serikali haioni sababu ya kuanzisha Idara au Kitengo Maalum cha Ufuatiliaji na Ushawishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kweli katika miradi hii 294 sababu ni swalii la takwimu naomba tutafute takwimu zaidi za uhakika na nitampa Mheshimiwa Mbunge ni miradi mingapi ambayo imetekelizwa kati ya hii 294.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii la pili tayari tuna vitengo vya ufuatiliaji kwa maana ya *Monitoring and Evaluation* katika Wizara, lakini pia hata katika taasisi zetu ikiwemo Kituo cha Uwekezaji cha TIC; na kwa taarifa tu katika miradi ambayo imetekelizwa mwaka 2021/2022 miradi zaidi ya 1,200 imeshafanyiwa ufuatiliaji kwa maana ya kuhakikisha kujua kama inatekelezwa na kwa kiwango gani. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji Mheshimiwa Yahaya Omary Massare Mbunge wa Manyoni Magharibi, sasa aulize swalii lake.

### Kuvuna Maji Katika Mji wa Itigi

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuvuna maji katika Mji wa Itigi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Yahaya Omari Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali inaendelea na ukarabati wa mabwawa mawili ya Rungwa na Muhanga yenye thamani ya zaidi ya milioni 460 yenye ukubwa wa kati katika Wilaya ya Manyoni ili kuongeza uvunaji wa maji ya mvua yatakayonufaisha wananchi katika Wilaya hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Omari Massare, swalii la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Swalii langu nimeulizia Mji wa Itigi ila imejibiwa vijiji. Basi, sasa je, Serikali ipo tayari sasa kuvuna maji katika Mji wa Itigi ili kujenga bwawa linaoitwa Mkalamani ambalo lipo palepale Mjini Itigi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kujibu swalii lake la nyongeza la kuvuna maji katika Mji wa Itigi.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Itigi ni moja ya Miji ambayo upatikanaji wake wa maji unaendelea vizuri kwa sasa ni zaidi ya asilimia 70. Kwa hiyo, kwenye masuala ya uvunaji wa maji tunazingatia zaidi maeneo ambayo maji yanapatikana kwa shida zaidi, lakini pale itakapobidi basi tutafanya hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa sasa aulize swalii lake.

Na. 153

### **Kesi za kodi kutoamriwa kwa wakati**

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Je, ni nini kinachosababisha kesi 1,097 za kodi za muda mrefu zenyet  
thamani ya shilingi trilioni 360 na dola za Marekani milioni 181.4 kutoamuliwa  
hadi sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemna, majibu.

## **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haina kesi 1,097 za kodi za muda mrefu zenyet thamani ya shilingi trilioni 360 na dola za Marekani milioni 181.4 ambazo haziqamuliwa.

Aidha, hadi Agosti, 2022 kulikuwa na mashauri 854 kwenye hatua mbalimbali za usikilizaji yenyе kodi inayobishaniwa ya jumla ya shilingi 4,207,442,214,759.93 (triliuni 4.21) na dola za Marekani 3,480,867.96 (milioni 3.48) katika Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi. Hivyo, kwa sasa taasisi za rufaa za kodi zinaendelea kusikiliza mashauri hayo pamoja na mashauri mapya yanayoendelea kusajiliwa.

Vilevile kwa nyakati tofauti, idadi ya mashauri ya kodi hupungua au kuongezeka kulingana na kasi ya usikilizaji na usajili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, swali la nyongeza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya CAG ya mwaka 2019/2020 na mwaka 2020/2021 kesi hizo nilizozitaja zimesajiliwa katika Mabaraza yetu; Baraza la Rufani za Kodi (*TRAT*) na Bodi ya Rufani za Kodi (*TRAB*) zilisajiliwa kesi hizi zenyet thamani ya trilioni 360 na hivyo kama majibu ya Serikali kwamba hakuna kesi ya trilioni 360 wakati kwa mujibu wa Taarifa ya CAG hizi kesi zilikuwa zimesajiliwa na Mabaraza haya; hizi kesi zipo wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, zipo taarifa za uhakika kwamba katika mwaka huu wa fedha Serikali iliamua kupokea shilingi bilioni 700 kuitia katika hiso kesi za shilingi trilioni 360 na katika kipindi cha Disemba, 2021 na Februari, 2022 Serikali ilipokea fedha hiso na kuzifuta kesi zenye thamani ya shilingi trilioni 360. Kwa nini Serikali iliamua kupokea fedha bilioni 700 badala ya shilingi trilioni 360 kama madai halali ya nchi? (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake aliyoyaleta, lakini naomba niweke kumbukumbu sawa; jambo hili hata jana nimeona limejadiliwa kwa kirefu sana na nitakuomba unipe dakika ili niweze kuliweka sawa.

Mheshimiwa Spika, jambo hili liko namna hii, ni kweli anachosema Taarifa ya CAG ya mwaka 2019 ilisema hivyo na Taarifa ya CAG ya mwaka 2019 maana yake ni ukaguzi wa vitabu vya mwaka 2018 (mwaka unaofuatia nyuma yake) lakini kilichofanyika ni kipi?

Mheshimiwa Spika, baada ya mzozo kujitokeza kati ya kesi ya Acacia pamoa na Serikali, Acacia aliiza jambo lile kwa Barrick na Rais wa wakati ule, Rais Magufuli aliunda timu ya kufanya makubaliano na hawa watu mwaka 2017/2018 na makubaliano hayo yaliendelea kwenye mjadala, yakaisha tarehe 24 Januari, 2020 na sherehe hizi zilifanyika lkulu mbele ya Rais Magufuli na shamrashamra kubwa na Tanzania tukakubali kuachilia shilingi trilioni 360 tumalize shauri lile na tukaunda Kampuni ya Twiga na nchi nzima tunasheherekea kampuni ile kwamba ina ubia wa asilimia 16 kwa Serikali na asilimia 84 kwa Barrick.

Mheshimiwa Spika, na mambo mengine yaliyokubaliwa kwenye makubaliano hayo la kwanza ni lile la ubia kwamba Serikali tutakuwa na asilimia 16 na wao watabakiza asilimia 84.

La pili, wao walikuwa na kesi na sisi ya dola bilioni 2.7 wakafuta kesi hiyo; la tatu, tukakubaliana kwamba watatoa dola milioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ambayo hata kwenye briefing ndio Mbunge wa Kahama aliyekuwa anaiulizia, tukakubaliana hilo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, tukakubaliana kwamba watakuwa wanatoa dola sita kwenye kila wakia ya dhahabu na tukakubaliana kwamba watatoa dola milioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya madini.

Kwa hiyo, haya yalikuwa sehemu ya *frame work agreement* ile ambayo ilikubalika na baada ya hapo tukawa tumeshamaliza yale mashauri yakiwemo na mengine ambayo yaliyokuwa yanahuisha mjadala kwenye makubaliano yale yaliyokuwa yanafanyika.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kuwa imeshafanyika hivyo, kilichofanyika kingine ilikuwa ni kuanza kupokea gawio baada ya kuwa jambo lile limeshafungwa.

**23 SEPTEMBA, 2022**

**SPIKA:** Dakika moja malizia kwa sababu tuko kwenye kipindi cha maswali na majibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, likawa limeshafungwa jambo hilo tangu mwaka 2020, kama lilishafungwa tangu mwaka 2020 kilichofuatia mwaka 2021 tulipokea gawio, mwaka 2022 tumepokea gawio na dola milioni 300 ambazo ndio kama bilioni 700 ilikuwa sehemu ya makubaliano kwenye mjadala uliofanyika na sherehe ile ilifanyika ikulu, mbele ya Rais Magufuli. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru sana. (Makofi)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mbona miongozo imekuwa mingi kuna mambo yamefanyika hapa nje ya kanuni sio? Haya ngoja nilete matangazo kwenu.

Kwanza ni tangazo la wageni walioko hapa Bungeni tutaanza na mgeni ambaye ameketi kwenye Jukwaa la Spika na maelezo yanayohusu mgeni huyu yameandikwa kwa lugha ya kingereza, kwa hivyo na mimi nitayasoma; Honorable Liam Dominic Byrne – Member of Parliament for Birmingham Hodge Hill, UK and the Global Chair of Parliamentary Network for the World Bank and IMF and also a Former UK Finance Minister, karibu sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge na wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana wageni wetu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wageni 31 ambaao ni Chama cha Majaji Tanzania kutoka Mikoa ya Simiyu na Shinyanga, karibuni sana wageni wetu, karibuni Bungeni. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, hilo ndio tangazo la wageni na tutaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc - KATIBU WA BUNGE:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**23 SEPTEMBA, 2022**

**NDG. JOSHUA CHAMWELA- KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) wa Mwaka 2022 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2022)**

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022**

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA-KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022**

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022**

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, miswada minne imesomwa hapa kwa mara ya kwanza na kwa utaratibu wetu miswada hii itaelekezwa kwenye Kamati zinazohusika na watakapokamilisha kazi watanitaarifu halafu italetwa hapa Bungeni ili Wabunge tuweze kujadili na pia kuweza kutunga sasa sheria juu ya hii miswada ambayo imesomwa mbele yetu. Kwa hiyo tutaipeleka kwenye Kamati zinazohusika.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA-KATIBU MEZANI:** Taarifa ya Katibu wa Bunge.

**SPIKA:** Katibu wa Bunge.

#### **TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc -KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya Mkutano wa Nane wa Bunge sasa zimemalizika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndio taarifa ya Katibu wa Bunge. Katibu!

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc -KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**SPIKA:** Hoja ya kuhairisha Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa aje awasilishe hoja kwa ajili ya kuhairisha Bunge. (Makofii)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema hadi leo tunapohitimisha shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano wa Nane wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulioanza kikao chake cha kwanza tarehe 13 Septemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kukushukuru wewe binafsi, kwa umahiri na uhodari wako katika kuongoza mijadala ya Mkutano huu wa Nane wa Bunge la Kumi na Mbili ukisaidiwa na Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, vilevile niwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yenyetija mliyoitoa wakati wa kuchangia hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali kwenye mkutano huu. Niwahakikishie kuwa michango, maoni na ushauri mlioutoa Serikali imepokea na inaadidi kufanya kazi kwa lengo la kujenga na kuimarisha utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, salamu za pole; siku za hivi karibuni tumeshuhudia kutokea kwa ajali mbalimbali za vyombo vya usafiri zikihusisha pikipiki, magari na kadhalika. Ajali hizo zimesababisha vifo vya wapendwa wetu, uharibifu wa mali na pengine ulemavu. Nitoe pole kwa Watanzania wenzangu waliopoteza wapendwa wao na wengine kupata majeraha kutohana na sababu mbalimbali ikiwemo matukio ya ajali za vyombo vya moto, niwatakie afya njema na uponyaji wa haraka wale wote waliojeruhiwa na kwa waliopoteza maisha tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahala pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa pia naungana na Watanzania wenzangu kutoa salamu za pole kwa familia ya Marehemu

Augustino Lyatonga Mrema, aliyekuwa Mwenyekiti wa chama cha *Tanzania Labour Party* aliyefariki tarehe 21 Agosti, 2022 jijini Dar es Salaam. Mchango wake katika mageuzi ya siasa, uzalendo na upendo aliokuwa nao nchini utaendelea kukumbukwa daima. Aidha, nitoe salamu za pole kwa familia ya Bi. Fatma Omar Latu aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora pamoja na dereva wake Bwana Alex Mtabika waliofariki kwa ajali ya gari tarehe 14 Septemba, 2022 wakiwa kazini wakitokea Mbeya. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nitoe pole kwa familia ya Mzee wetu Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na mtoto wake mpendwa Ndugu Hassan Ali Hassan Mwinyi aliyefariki tarehe 31 Agosti, 2022. Pia nitoe salamu za pole kwa familia ya Mheshimiwa Balozi Paul Rupia aliyefariki tarehe 16 Septemba, 2022 na ataagwa mchana wa leo pale Karimjee Jijini Dar es Salaam. Hakika mchango wake katika masuala ya kidiplomasia, mageuzi ya kiuchumi na utumishi wa umma hautosahaulika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki pia tumepokea kwa masikitiko vifo vyta viongozi mbalimbali duniani ikiwemo Hayati José Eduardo dos Santos, Rais Mstaafu wa Angola; Hayati Shinzo Abe, Waziri Mkuu Mstaafu wa Japan na Malkia Elizabeth wa Pili wa Uingereza. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Tamima Haji Abass, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum wa Chama cha Mapinduzi na kuungana nasi kwa ajili ya kuwawakilisha na kuwashudumia wananchi. Sisi Wabunge tunakukaribisha katika Bunge hili tukufu na tunakuhakikishia ushirikiano katika kutimiza majukumu yako ya kuwatumikia Watanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Septemba, 2022 Bunge lako tukufu lilifanya uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika ya Mashariki. Uchaguzi huo umewezesha kupata wawakilishi wetu tisa ambao ni Mheshimiwa Angela Charles Kizigha; Mheshimiwa Nadra Juma Mohamed; Mheshimiwa Dkt. Shogo Richard Mlozi; Mheshimiwa Dkt. Abdulla Hasnu Makame; Mheshimiwa Machano Ali Machano; Mheshimiwa Ansar Abubakar Kachwamba; Mheshimiwa James Kinyasi Milly; Mheshimiwa Dkt. Ng'waru Jumanne Maghembe; na Mheshimiwa Mashaka Khalfan Ngole. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuliwakilisha Taifa letu katika Bunge hilo. Ni matumaini yetu kuwa watakwenda kutimiza wajibu wa kulisemea Taifa letu na kusimamia maslahi mapana ya ukanda wa Afrika Mashariki katika kukuza uchumi na kuimarisha mshikamano mionganoni mwa nchi wanachama. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, shughuli za Bunge; katika mukutano huu, Bunge lako tukufu lilipata fursa ya kupokea maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na kutolewa majibu kutoka upande wa Serikali. Aidha, Bunge hili pia lilijadili na kupitisha miswada ya sheria na kuridhia maazimio mbalimbali ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Nane tunaouhitimisha leo, jumla ya maswali 153 ya msingi na maswali 468 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miswada ya Sheria, Bunge lako lilipokea, kujadili na kupitisha kwa hatua zake zote Miswada ya Sheria minne kama ifuatavyo: -

- i) Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022;
- ii) Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022;
- iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022; na
- iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua iliyofikiwa nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri na kuipitisha miswada hiyo wakati tukisubiri maamuzi ya Mheshimiwa Rais kuiidhinisha kuwa sheria kamili za nchi.

Mheshimiwa Spika, Miswada ifuatayo ilisomwa kwa mara ya kwanza katika Bunge lako tukufu:-

- i) Muswada wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania wa Mwaka 2022;
- ii) Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022;
- iii) Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022; na
- iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, vilevile Bunge lako tukufu lilifanikiwa kujadili na kuridhia maazimio mawili ya Bunge yafuatayo:-

- i) Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004; na

- ii) Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kuongeza Mamlaka ya Mahakama ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Kauli ya Serikali; Serikali imeendelea kufanya kazi masuala mbalimbali yanayohusu tozo ili kuhakikisha mapato na makusanyo yanaendelea kuimarishwa katika kuimarisha bajeti tulioipanga. Kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kushughulikia, kufanya tathmini na kufanya maboresho ya namna ambavyo tozo mbalimbali zinaweza kutekelezwa ili zilete manufaa kwa Taifa na kuwezesha maisha ya wananchi kuwa ya unafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, tarehe 20 Septemba, 2022 Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba aliwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu Kauli ya Serikali juu ya maboresho yaliyofanywa katika tozo za miamala ya kibenki. Nia ya Serikali ni kuendelea kufanya mapitio na tathmini juu ya mipango ya kukuza uchumi kupitia makusanyo ya kodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo iliwasilisha taarifa kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge pamoja na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge. Taarifa hiyo ilisheheni uchambuzi wa kina, maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa Serikali. Nitumie fursa hii kuwapongeza Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kazi nzuri waliyofanya kuanzia uchambuzi hadi kuwasilisha taarifa yao Bungeni. Serikali itafanya kazi ushauri na mapendekezo ya Kamati yaliyoletwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, maeneo ya msisitizo; pamoja na kuwa mkutano huu ulijikita katika kujadili na kupitisha miswada ya sheria na maazimio ya Bunge, naomba nitumie fursa hii kueleza kwa uchache kabisa na kusisitiza kama ifuatavyo; baadhi ya maeneo ambayo nitayatolea msisitizo ni suala la sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, usalama wa raia na mali zao, hali ya upatikanaji wa chakula na pembejeo za kilimo nchini na maandalizi ya mitihani ya kitaifa ya mwaka 2022. Maeneo mengine ni ada za mitihani zilizofutwa, upatikanaji wa mikopo ya elimu ya juu, uimarishaji wa miundombinu ya elimu ya juu, ujenzi wa Mji wa Serikali, lakini pia Umoja wa Mataifa, Mradi wa Bomba la Mafuta na michezo.

Mheshimiwa Spika, Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022; tarehe 23 Agosti, 2022 nchi yetu ilitekeleza zoezi la Sensa ya Watu na Makazi. Tumeshuhudia zoezi hilo likifanyika kwa amani na utulivu huku wananchi wakionesha ushirikiano wa hali ya juu. Kwa sasa zoezi limekamilika na Serikali inaendelea na uchakataji wa takwimu zilizokusanya. Nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi, taasisi na wananchi kwa kushiriki vizuri kwenye zoezi la Sensa ya Watu na Makazi. Aidha, niendelee kusisitiza matumizi sahihi ya takwimu za sensa mara zitakapotolewa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala la usalama wa raia na mali zao; vyombo vyetu vya usalama vimeendelea kusimamia hali ya usalama wa raia na mali zao. Hata hivyo, katika kipindi cha hivi karibuni, nchi yetu imepitia matukio kadhaa yaliyohusisha uhalifu na ajali za barabarani yaliyosababisha vifo na majeruhi.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa jamii, viongozi wa dini na Watanzania kuungana kwa pamoja kukemea, kufichua na kudhibiti matukio yote yanayoashiria kuondoa amani na utulivu wa nchi yetu. Aidha, nisisitize madereva na wamiliki wa vyombo vya moto hususani magari ya abiria kutambua dhamana waliyo nayo katika kulinda usalama wa abiria na watumiaji wengine wa barabara ili kuepusha ajali za mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, nilielekeze Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba linafuatilia matukio ya uhalifu na ajali za barabarani na kuyadhibiti kwa kushirikiana na jamii. Hivyo, elimu iendelee kutolewe na njia mbalimbali za ulinzi shirikishi katika kufichua uhalifu zitumike na ziimarishwe. Aidha, Jeshi la Polisi liendelee kuboresha mikakati yake ya kukabiliana na wimbi hili la uhalifu na ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine nizielekeze Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzia ngazi ya vitongoji, mitaa, vijiji, kata na wilaya kuhakikisha zinatimiza wajibu wa kudumisha amani, utulivu na utawala bora. Viongozi katika ngazi hizo wahakikishe kuwa mikutano ya kisheria inafanyika kama ilivyopangwa ili wananchi wapate fursa ya kupokea taarifa na kujadili mambo mbalimbali kuhusiana na ustawi wao ikiwemo masuala ya ulinzi na usalama. Suala la ulinzi na usalama liwe ni ajenda ya kudumu katika mikutano hiyo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo na hasa upatikanaji wa chakula nchini; katika kipindi cha mwaka 2021/2022 tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula imeonesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula umefikia tani milioni 17.4. Kati ya kiasi hicho uzalishaji wa mazao ya nafaka unaohusisha mahindi, mchele, mtama, uwele, ulezi na ngano, ni tani milioni 9.4 na mazao yasiyo ya nafaka ambayo ni jamii ya mikunde, mhogo, ndizi, viazi vitamu na mviringo uzalishaji ni tani milioni 7.9.

Mheshimiwa Spika, mahitaji yote ya chakula yanayojumuisha nafaka na yasiyo ya nafaka kwa mwaka 2022/2023 ni zaidi ya tani milioni 15 ambapo tani milioni 9.5 ni za mazao ya nafaka na tani milioni 5.5 ni mazao yasiyo ya nafaka. Kwa kulinganisha uzalishaji na mahitaji, nchi yetu ina kiwango cha utoshelevu wa chakula wa asilimia 115 na kuwa na ziada ya chakula kwa tani zipatazo milioni 2.3.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha utengamano wa hali ya chakula nchini unaendelea kuimarika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali. Hatua hizo ni pamoja na kuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kuhifadhi tani 147,142 na kuendelea kununua mazao ya chakula kwa ajili ya kuhifadhi. Nitumie fursa hii kutoa wito kwa wananchi kuendelea kuhifadhi akiba ya chakula tuliyonayo na kuwa na matumizi sahihi ya chakula.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa pembejeo; maandalizi ya msimu wa kilimo wa mwaka 2022/2023 yanaendelea sambamba na kuwezesha upatikanaji wa pembejeo muhimu hususani mbolea na dawa; na wastani wa matumizi ya mbolea nchini katika kipindi cha kati ya mwaka 2019/2020 hadi 2021/2022 umeendelea kuwa tani 430,000. Hadi kufikia tarehe 31 Agosti, 2022 upatikanaji wa mbolea nchini umefikia tani 213,403 sawa na asilimia 49.6 ya wastani wa matumizi ya mbolea.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa upatikanaji wa pembejeo katika kuongeza tija kwenye kilimo, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameridhia kutoa shilingi bilioni 150 ya ruzuku ya mbolea ili kuwezesha upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa wingi na kwa gharama nafuu. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2022/2023 utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima unalenga kuongeza uzalishaji wa chakula nchini na hivyo kuwa na usalama wa chakula na kukidhi upatikanaji wa malighafi za viwanda vya ndani. Hadi kufikia tarehe 31 Agosti, 2022 wakulima 956,920 wamesajiliwa kwa ajili ya kupata mbolea ya ruzuku ambapo jumla ya tani 60,882 za mbolea zimenunuliwa na wakulima katika mikoa ya Arusha, Iringa, Mbeya, Morogoro, Njombe, Rukwa, Ruvuma na Songwe. Nitumie fursa hii kuilekeza Wizara ya Kilimo kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima kwa wakati. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, sekta ya mifugo; mifugo ni miuongoni mwa sekta za kiuchumi ambazo ni muhimu katika kuondoa umaskini na kukuza uchumi. Sekta hii imeonesha ukuaji wa mwaka hadi mwaka na kuifanya Tanzania kuwa miuongoni mwa nchi zenyе mifugo mingi Barani Afrika. Hili limesababisha kuwepo kwa uhitaji mkubwa wa malisho ya uhakika pamoja na huduma bora za mifugo. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kuwa kila mfugaji anaafuata njia bora za ufugaji zitakazowezesha upatikanaji wa malisho ya uhakika na mifugo bora.

Mheshimiwa Spika, ufugaji usiozingatia uwezo wa eneo la malisho umechangia kwa kiasi kikubwa kuwa na tija ndogo katika sekta ya mifugo na kuwa chanzo cha migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi hususan wakulima. Hata hivyo, Serikali kwa kutumia mikakati mbalimbali kuititia mamlaka zake imekuwa ikitatua migogoro hiyo na kukomesha vitendo vinavyoikiuka taratibu za kisheria. Vilevile Serikali imechukua hatua mbalimbali za kutatua changamoto hizo ikiwemo kuboresha nyanda za malisho, ujenzi wa majosho, kudhibiti magonjwa, kutoa elimu ya uzalishaji wa mifugo na kuimarisha masoko ya bidhaa zitokanazo na mifugo.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu tutafute suluhisho la kudumu katika utatuzi wa migogoro baina ya wafugaji na wakulima. Hivyo nitumie fursa hii kuwaelekeza Mawaziri wa kisekta wakiwemo wa Mawaziri wa Mifugo na Uvuvi, Kilimo, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Maliasili na

Utalii, Mambo ya Ndani ya Nchi na Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kukutana na kutafuta namna bora ya kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya wafugaji na wakulima na kuja na suluhisho la kudumu. Sambamba na hilo nitoe wito kwa ndugu zetu wafugaji na wakulima kuishi kwa kufuata taratibu zilizowekwa katika mamlaka husika pale wanapotekeleza majukumu yao ya ufugaji na kilimo. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, vilevile naiagiza Wizara ya Mifugo na Uvuvi iendelee eneo la Msomera, Wilayani Handeni, Mkoani Tanga, kuwa ni eneo la mfano kwa ufugaji wa kisasa na wenye tija hapa nchini ili wafugaji nchini wapate kujifunza kutoka eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya elimu - maandalizi ya mitihani ya kitaifa mwaka, 2022; katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2022 wanafunzi wapatao milioni 1.7 wa darasa la nne, wanafunzi milioni 1.3 wa darasa la saba, wanafunzi 688,000 wa kidato cha pili na wanafunzi 537,000 wa kidato cha nne wanatarajiwaa kufanya mitihani yao kuanzia sasa mpaka mwezi Novemba. Maandalizi ya mitihani hiyo yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaelekeza watendaji wote wa elimu wakiwemo Maafisa Elimu wa Mikoa, Halmashauri, Wakuu wa Shule, Walimu na vyombo mbalimbali ambavyo vinahusika katika uratibu wa ufanyakaji wa mitihani hiyo ili kuzingatia sheria na taratibu za uendeshaji na usimamizi wa mitihani. Aidha, nitoe wito kwa wanafunzi kujiardaa kikamilifu na tunaendelea kuwaombea kila mmoja aweze kufanya mtihani wake na kuendelea kuwa na nidhamu wakati wote wa utendaji wa mitihani.

Mheshimiwa Spika, ada za mitihani zilizofutwa; Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanakamilisha mzunguko wa elimu na mafunzo katika ngazi husika kwa kuondoa vikwazo vitakavyosababisha wanafunzi kushindwa kukamilisha mzunguko wa elimu vikiwemo ada, michango na changamoto zinazotokana na mahitaji maalum kwa baadhi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huo, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameendelea kuondoa vikwazo vya ada na michango ambapo hivi karibuni ameridhia kufutwa kwa ada ya shilingi 50,000 kwa kila mtahiniwa wa kidato cha sita kwa shule za sekondari zinazomilikiwa na Serikali. Lengo la kufutwa kwa ada hiyo ni kuendeleza dhamira yake ya kuwapunguzia wazazi mzigo wa gharama za kuendesha elimu. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, elimu ya juu; Serikali imeendelea kuongeza wigo wa utoaji wa elimu ya juu nchini kwa kuhakikisha upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi unakidhi malengo. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga shilingi bilioni 570 kwa ajili ya wanafunzi wahitaji na wanaostahili

kupata mikopo, lakini vilevile shilingi bilioni tatu zitatolewa kwa ufadhili wa masomo (scholarship) kwa wanafunzi wenyewe ufaulu wa juu katika mitihani ya kidato cha sita watakaodahiliwa katika fani za hesabu, tiba, sayansi na uhandisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Taasisi za Elimu nchini. Kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (*HEET*) Serikali imetenga takribani shilingi bilioni 752, kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo: -

- i) Ujenzi na ukarabati; kujenga miundombinu mipyä ya ukarabati iliyopo ikiwemo kumbi za mihadhara na madarasa 130, maabara na karakana 108, mabweni 34 na ofisi 23.
- ii) Kuimarisha mafunzo kwa vitendo; Serikali inatarajia kukarabati na kuboresha miundombinu ya mashamba darasa na vituo atamizi kumi pamoja na kuweka vifaa vya kisasa vya TEHAMA katika vyuo vikuu na taasisi.
- iii) Ujenzi wa kampasi mipyä; Serikali imepanga kujenga kampasi mipyä 14 katika Mikoa ya Dodoma, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Manyara, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Simiyu, Singida, Shinyanga, Tabora na Tanga.
- iv) Ujenzi wa vyuo vikuu vipyä; Serikali imepanga kujenga Chuo Kikuu cha kisasa cha TEHAMA mkoani Dodoma na Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwl. Julius Nyerere Mkoani Mara.
- v) Kusomesha Wahadhiri; yako mahitaji ya wahadhiri kwenye vyuo vikuu vyetu na katika shahada za uzamivu na shahada za umahiri zitaendelea kupeleka wahadhiri wengi kwenda kusomea kwenye fani hizo, ili kuwajengea uwezo katika fani zao.
- vi) Lakini pia tutaimarisha utafiti; tutaendelea na kutafiti, kubiasharisha na kuwezesha matokeo ya tafiti na bunifu kutatua changamoto mbalimbali katika jamii.

Mheshimiwa spika, ujenzi wa Mji wa Serikali; awamu ya pili ya ujenzi wa Mji wa Serikali unaohusisha ujenzi wa majengo ya ofisi yenye urefu wa ghorofa kuanzia sita hadi tisa unaendelea vizuri. Hadi sasa ujenzi huo ambao ulioanza Oktoba, 2021umefikia wastani wa asilimia 50 na unatarajiwa kukamilika Oktoba, 2023.

Mheshimiwa Spika, mradi huu utakapokamilika utagharimu jumla ya shilingi bilioni 675.8 ambapo hadi sasa Serikali imetoea shilingi bilioni 250 na kiasi kilichobaki kitaendelea kutolewa kulingana na hatua za ujenzi ili kuwezesha mradi huo kukamilika kwa wakati. Aidha, mradi huu umenufaisha wakazi wa Dodoma na nije ya Dodoma ambapo hadi sasa jumla ya ajira 2,149 zimezalishwa katika maeneo ya wataalam, mafundi na vibarua.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa ofisi unaenda sambamba na ujenzi wa miundombinu mingine ya huduma za maji safi, maji taka, mawasiliano, TEHAMA, usalama, zimamoto na uokoaji na programu za upandaji miti. Aidha, katika mji huo kutakuwa na huduma mbalimbali za kijamii zikiwemo maeneo ya kupumzika, michezo, maduka makubwa (*shopping malls*), maeneo ya biashara, majumba ya cinema, nyumba za ibada, shule, hospitali, bustani za maua, vituo vya utamaduni na nyumba za makazi ya viongozi na watumishi waandamizi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara za lami zenyе urefu wa jumla ya kilometa 51.2 umekamilika kwa asilimia 99. Kazi zinazoendelea sasa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua, vituo vya mabasi, taa za barabarani, taa za kuongoza magari na barabara ya kuunganisha Mji wa Serikali na lkulu ya Chamwino.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaelekeza watendaji na wakandarasi wote kuhakikisha kwamba, utekelezaji wa mradi huu unakamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyokubalika. Aidha, nizikumbushe taasisi za umma zinazopaswa kuhamia Dodoma na hazijahamia zifanye hivyo mara moja.

Mheshimiwa Spika, Umoja wa Mataifa; sisi kama Taifa tunajivunia tunu tulizoachiwa na Waasisi wa Taifa letu ikiwemo tunu ya amani, umoja, utu, udugu na mshikamano mionganoni mwetu. Mtakubaliana nami kuwa tunu hizi zimekuwa ndio msingi wa uhai wa Taifa letu. Kwa kutambua umuhimu wa tunu hizi, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba Taifa letu linaendeleza kuzienzi tunu hizi ili kuwawezesha Watanzania kutekeleza majukumu yao bila hofu yoyote. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Rais akiwa katika maadhisho ya miaka 10 ya kumbukumbu ya Chuo cha Taifa cha Ulinzi, alilitangazia Taifa sera ya upatanishi, kuvumiliana, kuishi pamoja na kujenga nchi aliyoipa jina la R4 yaani *Reconciliation, Resiliency, Reforms and Rebuilding of the Nation*. Ni matarajio yake kuwa sera hii itabebwa na Watanzania wote ili sote twende pamoja kama Taifa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, maono na dhamira ya Mheshimiwa Rais ni kuendelea kutuunganisha Watanzania na kudumisha umoja wetu. Nami niungane naye kuwasisitiza Watanzania wenzangu kuendelea kuweka maslahi ya Taifa mbele ili kuwa na maendeleo kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo. Hivyo, nitoe rai kwa viongozi wa Serikali, viongozi wa dini, taasisi za elimu, maadili na utawala kuweka kipaumbele katika kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa sera ya upatanishi, kuvumiliana, kuishi pamoja na kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta; Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kusimamia kikamilifu sekta ya nishati nchini ili kukuza uchumi. Mheshimiwa Rais ana matamano makubwa ya kuifanya sekta ya nishati kuwa chanzo cha ukuaji wa uchumi na kuboresha sekta nyingine ikiwemo viwanda ambavyo ukuaji wake unategemea zaidi uwepo wa nishati ikiwemo mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga nchini Tanzania. Mradi huu ni muhimu kwa manufaa ya nchi zetu mbili katika kukuza biashara, viwanda vya uzalishaji, kuongeza ajira pamoja na kuvutia wawekezaji ambao wanatarajia kukuza teknolojia na ujuzi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wadau wa maendeleo wamekuwa na mashaka katika kuendeleza mradi huu wakihofia kuwa unaweza kutekelezwa pasipo kuzingatia athari za kimazingira na haki za kibinadamu. Mradi huu umefanyiwa tathmini ya kina ya kimazingira na kuhakikisha kuwa utekelezaji wake hauna athari za kimazingira na kwa jamii. Mradi huu kwa upande wa Tanzania unagusa watu 9,513 ikiwemo taasisi mbalimbali. Miiongoni mwao ni watu 331 pekee ndio watakaohamishwa sawa na asilimia 3.5.

Mheshimiwa Spika, wanaoguswa na mradi huu wanashirikishwa kuchagua kujengewa makazi mapya au kupewa fedha taslimu. Hata hivyo asilimia 85 walichagua kujengewa makazi. Hivyo ujenzi wa makazi hayo unaendelea ambapo nyumba 37 kati ya 309 zimekamilika na kukabidhiwa kwa wahusika. Aidha, nyumba 55 zipo kwenye hatua mbalimbali za umalizaji na nyumba 217 zipo kwenye hatua mbalimbali za awali za ujenzi wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaungana na Serikali ya Jamhuri ya Uganda kuwahakikishia wadau wote likiwemo Bunge la Umoja wa Ulaya na Jumuiya ya Kimataifa kuwa mradi huu unatekelezwa kwa kuzingatia sheria zote za Tanzania na Kimataifa, uwazi, tahadhari za kimazingira, ulinzi wa mifumo ya kiikolojia na rasilimali za maji, masuala ya kijamii, kijinsia na haki za binadamu kwa ujumla yote haya yanazingatiwa kwenye mradi huu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, hivyo niwatoe hofu wadau wote kuhusiana na utekelezaji wa mradi huu na Serikali itaendelea kutumia njia za kidiplomasia kuhakikisha kuwa wadau wanapata taarifa sahihi kuhusu utekelezaji wa mradi huu unaozingatia viwango vyote vya kimataifa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, michezo; kwa upande wa michezo nitumie fursa hii kuzipongeza timu zetu za mpira wa miguu za wanaume na wanawake kwa kuendelea kupeperusha vyema bendera yetu ya Taifa katika mashindano mbalimbali ya kimataifa. Nianze kwa kuzipongeza timu zetu za wanaume za

Simba na Yanga kwa kufuzu katika hatua ya awali ya michuano ya Klabu Bingwa Barani Afrika. Timu ya Simba iliifunga timu za Nyasa Big Bullets nyumbani na ugenini kwa jumla ya magoli 4-0, huku timu ya Yanga ikiichabanga timu ya Zalan nyumbani na ugenini kwa jumla ya magoli 9 - 0. Hongereni sana! (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine niipongeze timu ya Kipanga kutoka Visiwani Zanzibar ambayo imefuzu hatua ya awali ya mashindano ya Shirikisho Barani Afrika kwa kuifunga timu ya Ah Hilal Wau na timu ya Azam ambayo inasubiri hatua ya kwanza ya mashindano hayo. Pia, kipekee nitambue juhudji kubwa iliyooneshwa na timu zetu za KMKM na Geita Gold Mining katika kupambania kufuzu hatua ya awali ya mashindano ya Shirikisho, lakini walipoteza michezo yao. Hii iendelee kuwa chachu ya kuhakikisha timu zetu zinaendelea kuandaliwa vizuri na kupata uwakilishi na kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua juhudji kubwa za Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kukuza michezo na hasa mpira wa miguu wakiwemo wanawake, matokeo chanya yameanza kuonekana. Hii ni baada ya timu ya wanawake ya Simba Queens kutwaa ubingwa wa CECAFA na kufuzu mashindano ya Klabu Bingwa Afrika kwa Wanawake. (Makofij)

Nitumie nafasi hii kuipongeza sana Simba Queens kwa ushindi na nawatakia kila la heri katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika yatakayofanyika nchini Morocco. Aidha, niipongeze Timu ya Taifa ya Wanawake (*Twiga Stars*), kwa kushika nafasi ya tatu katika mashindano ya COSAFA yaliyofanyika nchini Afrika Kusini. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, ukuaji katika sekta ya michezo umeendelea kuimariika kwani tumeona aina nyingine ya michezo ikiwemo masumbwi na riadha ikiendelea kukua na kuleta mafanikio, lakini pia na kupeperusha bendera ya nchi yetu. Hapa msisitizo ni kuhakikisha kwamba nchi yetu inatambulika kwenye medani za dunia kwenye michezo.

Mheshimiwa Spika, pia, nizitakie heri Timu zetu za Taifa ikiwemo Timu ya Taifa ya Walemaru ya Mpira wa Miguu (*Tembo Warriors*) ambayo itashiriki Kombe la Dunia mwezi Oktoba, 2022 nchini Uturuki na Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 17 (*Serengeti Girls*) ambayo itashiriki michuano ya Kombe la Dunia nchini India mwezi Oktoba, 2022. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, nami nitumie nafasi hii kuzitakia maandalizi mema timu zetu za Bunge ikiwa ni kujiweka tayari kwenda kwenye mashindano ya Mabunge ya Afrika Mashariki itakayochewa nchini Sudan Kusini mwezi Novemba na Disemba, 2022. Timu za Bunge zikumbuke kuwa zinazo wajibu wa kulinda makombe yote saba tunayoyashikilia toka mwaka 2021. Tunawatakia kila la kheri. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, hitimisho; wakati naelekea kuhitimisha hotuba yangu, nitumie fursa hii kukupongeza wewe na Bunge lako tukufu kwa kushiriki katika Mkutano wa 51 wa Jukwaa la Mabunge ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC Parliamentary Forum*) uliofanyika Lilongwe nchini Malawi kuanzia tarehe 11 hadi 16 Julai, 2022. Aidha, nipongeze kwa hatua ya Bunge letu kushiriki Mkutano wa 65 wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola uliofanyika Halifax, nchini Canada kuanzia tarehe 23 hadi 25 Agosti, 2022 ambapo tuliwakilishwa na Wabunge Wawakilishi wa tawi la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Bunge lako tukufu kwenye mikutano hiyo, ni ishara tosha ya utekelezaji mzuri wa diplomasia yetu ya Mabunge yaani *Parliamentary Diplomacy* ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kuimarisha ushirikiano wa Bunge lako tukufu na mabunge mengine ya Kimataifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia, nimshukuru Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kazi kubwa ya kuratibu vikao vyta mkutano huu. Aidha, niwashukuru watendaji wa Serikali kwa kufanikisha shughuli zilizopangwa na Bunge lako tukufu kwa weledi na ufanisi mkubwa. Vilevile nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watendaji wake wote kwa kazi kubwa waliyoifanya katika mkutano huu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kipekee, niwashukuru sana wanahabari kwa kufikisha habari kuhusu mkutano huu na mengine kwa wananchi. Nivishukuru pia vyombo vyta ulinzi na usalama kwa kuimarisha ulinzi wakati wote, bila kuwasahau madereva wetu wanaofanya kazi kubwa sana kutuendesha kutuleta hapa na wanaturudisha makwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwatachia safari njema Waheshimiwa Wabunge, niwaombe mnaporejea majimboni kwenu muendelee kuwahamasisha wananchi na kuwahabarisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuiunga mkono Serikali yao kwenye jitihada zake za kujenga uchumi imara, wenyewe ushindani na kujitegemea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tarehe 8 Oktoba 2022 kutegemea mwandamo wa mwezi, ndugu zetu Waislamu wanatarajia kuadhimisha Mazazi ya Mtume Muhammad - *Swalla Allahu Alayh Wasallam*. Hivyo, niwatakie maandalizi mema na kheri katika maadhimisho ya shughuli hiyo ya Maulid.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kutoa hoja kuwa Bunge lako tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 1 Novemba, 2022 saa tatu kamili asubuhi tutakapokutana tena katika ukumbi huu jijini Dodoma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. (Makofi)

**23 SEPTEMBA, 2022**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja imetolewa lamuliwe)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na karibia Bunge zima. Wale waliokaa ni kwamba, hawataki kutoka hapa Dodoma. (Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, asanteni sana. Sasa nitawahoji kwqa mujibu wa taratibu zetu; Wabunge wanaofiki hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuahirisha Bunge mpaka tarehe 1 Novemba, 2022. (Makofi)

(Hoja liiamuliwa na Kuafikiwa)

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:** Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**SPIKA:** Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### **WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRICA MASHARIKI**

(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliimbwa)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae kwa ajili ya matangazo kidogo.

Kwanza nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na kumpongeza kwa hotuba aliyoitoa mapema muda huu ya kuahirisha Bunge ameeleza kwa kifupi lakini kwa ufasaha mambo yote ambayo Bunge tumeshayafanya, lakini pia katika kipindi hiki maamuzi ambayo Serikali imeyafanya katika maeneo mbalimbali na mambo ambayo yametokea nchini kwa ujumla, kwa hiyo tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (Makofi)

Lakini pia nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge pamoa na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri mliyoifanya kipindi chote ambacho sote tulikuwa hapa Dodoma, mlianza na Kamati na baadaye kukutana humu ndani kila Mbunge amefanya kazi nzuri sana kwa sehemu yake nawapongeza sana. (Makofi)

Nichukue pia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, kwa kazi nzuri ya usaidizi aliyoifanya katika kipindi hiki na anayoendelea kuifanya na pia Wenyeviti wawili wa Bunge

ambao wameendelea kufanya kazi kwa weledi mkubwa nao ninawashukuru sana Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa David Kihenzile. Ninawashukuru sana. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo iko Miongozo ambayo iliombwa na Waheshimiwa Wabunge ambayo iliombwa katika Bunge hili kwa hivyo inabidi isemwe katika Bunge hili; kwanza kabisa ni Mwongozo ambao nilisema mimi ningetua maelezo juu ya malalamiko aliyokuwa ameyatoa Mheshimiwa Almas Maige kuhusu kutojibiwa kikamilifu kwa swali lake. Kwa hali ya kawaida huwa nasoma kwa kirefu Mwongozo mzima ili mtu apate picha, lakini kwa sababu tunao utaratibu kikanuni wa kuingiza Taarifa Rasmi za Bunge basi nami nitatumia fursa hiyo kwamba Mwongozo huu nitausema tu sehemu, lakini Mwongozo wote utaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge na kwa hivyo Mbunge yeoyote atakayetaka kujua maamuzi niliyoyatoa kuhusu jambo hili kwa kirefu atawezza kupitia Taarifa Rasmi za Bunge.

Sasa hiyo kwa sehemu ambayo nimesema nitaizungumza kwa sababu niliahidi kuhusu swali lake ambalo aliliuliza hapa ndani niliahidi na kuelekeza kwamba swali la Mheshimiwa Maige lingeweza kuulizwa upya endapo lingekuwa halijajibiwa kikamilifu.

Baada ya kujiridhisha kuwa lilijibiwa kikamilifu uamuzi wangu ni kuwa Mheshimiwa Maige kwa sababu hakupewa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza kwa sababu ya maelezo aliyokuwa ameyatoa mwanzo na ndiyo yaliyonipelekea kwamba nitaleta maelezo hapa swali lake lilijibiwa kikamilifu na Serikali ila kwa kuwa hakupata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza lile swali litarejea kwenye Bunge lijalo kwa kadri ya majibu ya Serikali vile vile yalivyokuwa halafu Mheshimiwa Maige atapewa fursa ya kuuliza maswali yake ya nyongeza. Kwa hiyo huo ndiyo muongozo wangu kuhusu majibu aliyokuwa amepewa Mheshimiwa Maige na Serikali yalikuwa sahihi na yalikuwa yanajitosheleza kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 53.

**MWONGOZO WA SPIKA JUU YA MALALAMIKO YA MHE. ATHUMAN A. MAIGE  
(MB) KUHUSU KUTOJIBIWA KIKAMILIFU KWA SWALI LAKE – KAMA  
ULIVYOANDALIWA**

---

**Waheshimiwa wabunge**, Tarehe 13 Septemba 2022 katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Nane wa Bunge, Mhe. Athuman A. Maige, Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini, aliliza swali la msingi namba 7 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwamba,

*“Je ni lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa Sheria ya Kampuni Binafsi za Ulinzi?”.*

Swali hilo lilijibiwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Hamad Masauni (Mb) kama ifuatavyo:-

“Mhe Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa Sheria inayosimamia Makampuni Binafsi ya Ulinzi na kwa sasa waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mapendekezo ya kutunga Sheria ya Huduma za Sekta Binafsi ya Ulinzi umekamilika na utawasilishwa katika baraza la Mawaziri kwa ajili ya maamuzi baada ya kupata maoni ya wadau wa pande zote za Muungano juu ya Rasimu ya Sheria hiyo. Baada ya kukamilika kwa hatua hizo, Muswada wa Sheria hiyo utaletwa Bungeni.”

**Waheshimiwa Wabunge**, mara baada ya kuuliza swali la Msingi, nilimpatia Mhe. Maige fursa ya kuuliza Maswali Mawili ya nyongeza ambapo aliuliza kama ifuatavyo:-

“Mhe Spika, kwanza naomba nisikitike kwamba **majibu ya Serikali hayaridhishi**. Muswada huu niliuleta mimi binafsi mwaka 2016 ndio ukachukuliwa na Serikali. **Hii ni Mara ya tatu, Serikali inajibu hivi hivi** kwamba inafanya hivi inapeleka kwa wadau, Je, Serikali haionti kwamba miaka sita kungojea muswada mmoja ni muda mrefu sana?”

“Mhe Spika, Swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari sasa kuruhusu mjadala kati ya mimi niliyeleta muswada huo ili kuukwamua muswada huo?”

**Waheshimiwa Wabunge**, baada ya Maswali hayo, Kiti kilimtaka Mhe. Maige kutoa ufanuzi kutokana na Swali lake Kwanza la Nyongeza lililooniesha kuwa majibu ya Mhe. Waziri hayana uhalisia, na haridhiki nayo. Mh Maige alilalamika kuwa, kwa mara ya tatu amekuwa akipewa majibu hayo hayo na hiyo ndio sababu ya kutoridhika na majibu hayo.

Katika kutafakari suala hili nimejiuliza Maswali kwamba, Je, majibu ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Swali Na. 7 lilioulizwa na Mhe. Maige (Mb) yalikuwa hayaridhishi, hayana ukweli na hayakuwa na uhalisia kama ilivyolalamikiwa na Mhe. Maige? na Je, iwapo hakujibiwa kikamilifu nini kifanyike?

**Waheshimiwa Wabunge**, nimepitia Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) ili kuona majibu yaliyotolewa na Waziri kwenye Swali la Msingi na vile vile nimeangalia Swali Na. 7 lilioulizwa na Mhe. Maige (Mb) pamoja na Kanuni ya 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020 ili kujiridhisha na malalamiko yaliyotolewa na Mhe. Maige

**Waheshimiwa Wabunge**, Swali la Msingi la Mhe. Maige (Mb) lilitaka kujua ni lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa Sheria ya Kampuni Binafsi za Ulinzi.

Majibu ya Mhe. Waziri kwa Swali hilo wakati akitoa ufanuzi alieleza kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa Sheria ya Huduma za Sekta Binafsi ya Ulinzi. Waziri alieleza zaidi kuwa Serikali inaendelea kulifanya kazi jambo hilo ambapo limefikia ngazi ya Baraza la Mawaziri ambako wanaendelea na mchakato.

**Waheshimiwa Wabunge**, kutokana na malalamiko ya Mhe. Maige kupitia Swali lake la Kwanza la Nyongeza kwamba, Majibu ya Mhe. Waziri hayakumridhisha, nimejielekeza kwenye masharti ya Kanuni ya 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020. Kanuni hii imeweka masharti ya Swali linaloulizwa kujibiwa kikamilifu.

**Waheshimiwa Wabunge**, baada ya kuyasikia Malalamiko ya Mhe. Maige kwamba majibu ya Waziri hayakuwa kamilifu na kuwa Swali la Msingi halikujibiwa kikamilifu. Baada ya maelezo ya Mhe. Maige (Mb) ambayo aliyatoa kabla ya kuuliza maswali yake ya nyongeza niliahidi kufuatilia suala hilo kwa kuangalia Taarifa Rasmi za Bunge ili kujiridhisha kama Waziri alijibu sawa sawa ama tofauti, na iwapo ni tofauti, basi Mhe. Maige apatiwe fursa ya kujibiwa Swali lake wakati mwingine.

**Waheshimiwa Wabunge**, baada ya kuzingatia Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) na kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020 nimeridhika kuwa Majibu yaliyotolewa na Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi kwa Swali la Msingi Namba 7 la Mhe. Maige (Mb) yalikuwa ya kuridhisha, yaliendana na Swali la Msingi na yalikuwa na Uhalsia.

**Waheshimiwa Wabunge**, hata hivyo, kwa kuwa Mhe. Maige (Mb) alianza kulalamika kabla ya kuuliza maswali yake ya nyongeza nilimkatisha ili kujiridhisha kwanza juu ya uhalsia wa malalamiko yake hivyo, ninaona ni vema aitumie fursa hiyo. Kwa hiyo basi, naelekeza kwamba swali la msingi Na. 7 la Mhe. Maige (Mb) liulizwe upya na lipate majibu ya Serikali katika Mkutano wa Tisa wa Bunge. Aidha, Mhe. Maige (Mb) atapewa fursa ya kuuliza maswali yake mawili ya nyongeza.

Huo ndio Mwongozo wa Spika.

Umetolewa leo tarehe 23 Septemba, 2022

Mhe. Dkt. Tulia Ackson (MB)

**SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, lakini pia uliombwa muongozo mwingine katika Bunge hili na Mheshimiwa Halima James Mdee kuhusu kutojibiwa kikamilifu kwa maswali yake ya nyongeza katika swali lake namba 105.

Waheshimiwa Wabunge kama maelezo niliyoyatoa hapo awali muongozo huu pia utaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge na Mbunge yeyote ama mwananchi yeyote atakayetaka kusoma kwa kirefu kuhusu mwongozo huu ataupata hapo.

Lakini kwa kifupi aina ya swali na namna liliyokuwa limeulizwa na Mheshimiwa Halima Mdee lile alilosema halikujibiwa, lilikuwa linahitaji jibu la ndiyo au hapana na kwa kulikosa jibu hilo Mheshimiwa Mdee aliona kwamba swali lake halikujibiwa kikamilifu. Lakini kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yalitolewa kwa ujumla wake kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inafanya jitihada za kulipa madeni ninaona swali hilo lilijibiwa kikamilifu.

Hivyo basi maswali ya nyongeza yalipata majibu kikamilifu na sitatoa maelezo ya kutaka maswali hayo yajibewe upya kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 53 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za 2020.

Kwa hivyo, baada ya kutafakari maombi hayo ya muongozo wa Mheshimiwa Halima Mdee Taarifa Rasmi za Bunge pia nikazipitia na masharti ya Kanuni hiyo ya 53 nimeridhika kuwa majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwenye maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Halima James Mdee yajibowi kikamilifu na yaliendana na namna yeche aliyyouliza maswali yake.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge miongozo hii miwili imeshatolewa majibu yake hapa.

**MWONGOZO WA SPIKA ULIOOMBWA NA MHE. HALIMA JAMES MDEE (MB)  
KUHUSU KUTOJIBIWA KIKAMILIFU KWA MASWALI YAKE YA NYONGEZA KATIKA  
SWALI NAMBA 105 – KAMA ULIVYOANDALIWA**

---

**Waheshimiwa Wabunge**, tarehe 21 Septemba, 2022 katika Kikao cha Saba cha Mkutano wa Nane wa Bunge, Mhe. Halima James Mdee, (MB), aliomba Mwongozo wa Spika kwa maelezo kwamba Maswali yake mawili ya nyongeza hayakujibiwa kikamilifu na Mhe. Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**Waheshimiwa Wabunge**, Mhe. Mdee (Mb) aliuliza Swali la Msingi Namba 105 katika Wizara ya Fedha na Mipango kwamba;

“Je, ni lini Serikali italipa madai ya Shilingi Trilioni 7.91 ya watoa Huduma kama yalivyoripotiwa kwenye Ripoti ya CAG 2021?”

Swali hilo lilijibiwa na Naibu Waziri kama ifuatavyo (nanukuu)-

"Mheshimiwa Naibu Spika, deni la Shilingi Trilioni 7.91 linajumuisha madeni ya Wafanyakazi na Watoa huduma kwa Mashirika ya umma 71. Ili kuhakikisha madeni hayo yanalipwa na kudhibiti uzalishaji wa madeni mapya, Mashirika yote ya Umma yameelekezwa kuendelea kulipa kwa haraka iwezekanavyo na kuanda mkakati wa kukabiliana na Madeni na kuwasilisha Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkakati huo, kila Taasisi inatakiwa kuonesha namna itakavyodhibiti uzalishaji wa madeni mapya na kulipa madeni yaliyopo. Lengo ni kuhakikisha kuwa kiwango cha madeni kinafikia asilimia mbili ya jumla ya bajeti ya Mashirika ya Umma ifikapo Mwaka 2025. Aidha Ofisi ya Msajili wa Hazina na Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali itatumia mkakati huo katika uchambuzi na uidhinishaji wa mapato na matumizi ya kila Mwaka. Ahsante." (Mwisho wa kunukuu).

**Waheshimiwa Wabunge**, Mhe. Halima Mdee (Mb) aliruhusiwa kuuliza maswali mawili ya nyongeza ambapo aliuliza (nanukuu)-

"Mheshimiwa Naibu Spika, kwakuwa madeni haya Shilingi Trilioni 7.9 kama uliyosema ni ya Wafanyakazi, Watoa Huduma na Wauzaji bidhaa na ni ya muda mrefu, hauoni kwamba Serikali mnakuwa sehemu ya kufifisha shughuli za kiuchumi za Watanzania?, Swalii la kwanza"

"Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Wizara yako ya Fedha ndiyo inayomsimamia Msajili wa Hazina sasa ni lini mkakati huu utakamilika, nataka time frame ili mkakati huu upelekwe kwenye Kamati ya Bunge inayosimamia Mashirika ya Umma kwa ajili ya ufuatiliaji na utekelezaji? Ni lini? Time Frame?

Mhe. Naibu Waziri alijibu maswali hayo, pamoja na mambo mengine alisema (nanukuu)-

"Mipango ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tumelipa madeni yote hasa Serikali ya Awamu ya Sita, tumelipa madeni yote yaliyopo katika Serikali, lakini ni lini mkakati huu utaanza kutumika ni wakati wowote baada ya kupitia na kuhakiki wataalam wetu basi itatolewa taarifa rasmi. Ahsante." (Mwisho wa kunukuu).

**Waheshimiwa Wabunge**, kutokana na majibu hayo Mheshimiwa Mdee aliomba Mwongozo wa Spika akieleza pamoja na mambo mengine kuwa Mhe. Naibu Waziri hakujibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ambavyo Kanuni ya 53(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 inayoweka masharti kwa Waziri anayeulizwa Swalii kujibu kikamilifu. Baada ya maombi hayo ya Mwongozo, nilieleza kuwa nitapitia hansard ili kujiridhisha

iwapo Maswali hayo yamejibiwa kikamilifu ili kuniwezesha kutoa maelekezo kwa mujibu wa Kanuni. Nimepitia Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) na nimeona Maswali ya nyongeza ya Mhe. Mdee Pamoja na Majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri.

**Waheshimiwa Wabunge,** Maswali ya Nyongeza ya Mhe. Halima Mdee (Mb) yalitaka kujua mambo mawili, moja, Naibu Waziri haoni kwamba, Serikali inakuwa sehemu ya kufifisha Shughuli za kiuchumi za Watanzania? Pili, Ni lini Mkakati wa Serikali na Msajili wa Hazina kulipa madeni utakamilika? Majibu ya Mhe. Naibu Waziri kuhusu Mkakati wa Serikali unaosimamiwa na Msajili wa Hazina wa kulipa Madeni, alieleza kuwa, utaanza kutumika wakati wowote baada ya wataalam kukamilisha uhakiki. Naibu Waziri alieleza zaidi kuwa, mara baada ya mkakati huo kukamilika Serikali itatoa taarifa. Kwa majibu hayo, nimeridhika kuwa Swalii hili la Nyongeza lilijibiwa ipasavyo. Muuliza Swalii alitaka kujua muda ambao Mkakati utaanza kutumika na alijibiwa kwamba Serikali inafanya kazi jambo hilo, na alieleza zaidi kuwa baada ya uhakiki kukamilika Serikali itatoa taarifa.

**Waheshimiwa Wabunge,** Swalii la kwanza lilitaka kupata maoni ya Waziri iwapo Serikali inahusika kufifisha Shughuli za kiuchumi za Watanzania. Katika kutoa jibu la Swalii hilo, Naibu Waziri alitoa ufanuzi kwa ujumla kwamba, Serikali ina mipango ya kuhakikisha inalipa madeni yote yanalipwa.

**Waheshimiwa Wabunge,** Aina ya hii ya Swalii na namna liliyyoulizwa, linahitaji jibu la nadio au Hapana na kwa kulikosa jibu hilo, Mhe. Mdee ameona Swalii lake halijajibiwa kikamilifu. Lakini kwa kuwa majibu ya Mhe. Naibu Waziri yalitolewa kwa ujumla wake, kwamba Serikali ya awamu ya sita inafanya jitihada za kulipa madeni, ninaona Swalii hilo lilijibiwa kikamilifu. Hivyo basi, Maswali ya nyongeza yalipata Majibu kiukamilifu, sitatoa maelekezo ya kutaka Maswali hayo yajibiwe upya kwa mujibu wa Kanuni 53(4) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Waheshimiwa Wabunge,** baada ya kutafakari maombi ya Mwongozo alioombwa na Mhe. Mdee, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) na Masharti ya Kanuni ya 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020 nimeridhika kuwa Majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwenye maswali mawili ya nyongeza ya Mhe. Halima Mdee yaliyibiwa kikamilifu, yaliendana na namna Maswali hayo yalivyoulizwa.

Huo ndio Mwongozo wa Spika.

Umetolewa leo tarehe 23 Septemba, 2022

Mhe. Dkt. Tulia Ackson (MB)  
**SPIKA**

**SPIKA:** Lakini ninalo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa ameweka kwenye vishkwambi vyetu Jarida la Bunge Toleo la Nne la mwezi Juni, 2022 kwa hiyo mtalikuta kwenye vishkwambi vyenu na Jarida hilo limeangazia shughuli za Kamati za Bunge pamoja na Mkutano wa Bunge la Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Aidha, Jarida hilo pia limesheheni makala mbalimbali elimishi kuhusu shughuli za Bunge pamoja na ushiriki wa Bunge kwenye mikutano mbalimbali ya kimataifa. Ni muhimu Waheshimiwa Wabunge tupitie Jarida hilo kwa sababu lina taarifa nyingi muhimu.

Sasa hapa walikuwa wamesimama Wabunge wawili wakiomba muongozo ambao ulikuwa unaashiria kwamba kuna jambo ambalo limefanyika hapa Bungeni ambalo halijafuata utaratibu ama halijafanyika kikanuni.

Sasa kwa sababu ukiomba mwongozo ni hoja inayohusu Kanuni, itakuwa mtihani kidogo tukifunga Bunge watu wakajua kwamba kuna kanuni zimevunjiwa hapa, kila mmoja wenu anapewa dakika moja aeleze ni namna gani anataka kujua hilo jambo kama linaruhusiwa au haliruhusiwi Mheshimiwa Swalle, Mheshimiwa Neema dakika moja moja kila mmoja.

Mheshimiwa Neema Lugangira, Mheshimiwa Swalle naona umeshasimama, Mheshimiwa Enos Swalle

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niliomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 76 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 53 kuhusu jambo ambalo lilikuwa limetokea mapema asubuhi.

Nilikuwa nimeuliza leo swali namba 138 ambalo limejibiwa na Serikali ndani ya Bunge na baada ya hapo nikawa na maswali mawili madogo ya nyongeza ambayo kwa jinsi ambavyo nilikuwa nimeuliza hayakujibiwa kwa ufasaha kinyume na Kanuni ya 53 na maelezo ni kwamba swali la kwanza nilikuwa nimeomba kujua ni lini Serikali italeta Bungeni sheria ya kuweka ukomo wa makosa ya jinai ambayo yanakaa muda mrefu sana mahakamani bila kuisha; na majibu yake yakawa ni kwamba Serikali imeweeka sheria ya kutokufungua mashauri mpaka upelelezi upatikane lakini ukweli ni kwamba yako mashauri mengi yako mahakamani yanakaa miaka mingi hayaishi. Nilikuwa nataka kujua kwa nini Serikali isilet sheria Bungeni haya mashauri yawe na ukomo.

**SPIKA:** Sawa hoja yako imeeleweka kwamba maswali yako ya nyongeza hayakujibiwa kikamilifu si ndiyo hoja yako? Imeeleweka.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Umeeleweka Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nami nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 76 pamoja na ile Kanuni ya 53.

Mheshimiwa Spika, mapema leo niliuliza swali namba 139 lakini maswali yangu ya nyongeza mawili hayakupata majibu ya Serikali kwa ufasaha na nasema hivi kwa sababu mimi niliuliza maswali kwa msingi wa makosa ya jinai yenyé dhamana kwa sababu naamini ya kwamba tunapongelea makosa ya jinai yapo makosa yenyé dhamana na yapo makosa ambayo hayana dhamana.

Kwa hiyo, mimi nililenga makosa yenyé dhamana kwa maana ya kwamba Serikali iweke ukomo wa upetelezi kwenye makosa yenyé dhamana, lakini pili Serikali ibadilishe au iboreshe masharti ya dhamana kwa sababu watu wengi ambao wako mahabusu ni wale ambao wamefanya makosa yenyé dhamana, lakini wanashindwa kukidhi masharti yale ya dhamana. Ahsante.

**SPIKA:** Sawa kwa hiyo hoja yako na wewe swali halijajibwa kikamilifu

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, sahihi.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge wamesimama Wabunge wawili hapa wakiashiria kwamba maswali yao hayajajibwa kikamilifu na wote wametumia Kanuni ya 76 wakitaka kujua kama jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Kimsingi hairuhusiwi kutokujibu maswali ya Wabunge kikamilifu maswali ya Waheshimiwa Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi lazima yajibiwe kikamilifu. (Makofii)

Kwa hiyo, hiyo ni sehemu ya kwanza ya mwongozo huu, lakini Waheshimiwa Wabunge kwa sababu majibu yaliyotolewa na namna maswali yalivyoulizwa lazima nikajiridhishe, kwa hivyo miongozo hii miwili mtaniwia radhi sitaweza kuitoa kwenye Bunge hili, lakini nitaitoa kwenye Bunge lijalo na kama kutakuwa na sababu basi majibu yatasolewa wakati huo ikiwa haya maswali yatajibwa upya tutakuwa tumeyasema wakati huo na yatapangiwa katika Bunge hilo hilo lijalo na kama yatakuwa yamejibwa kikamilifu basi pia Waheshimiwa Wabunge mtajulishwa kwamba maswali hayo yamejibwa kikamilifu.

Kwa hiyo, mwongozo wangu ni kwamba majibu lazima yatolewe majibu ambayo yanatoa majibu halisi kwa Waheshimiwa Wabunge lakini kwa sehemu ya pili ya miongozo waliyoomba tutayatazama Taarifa Rasmi za Bunge.

## **23 SEPTEMBA, 2022**

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninawatakia kila la heri Waheshimiwa Wabunge safari zenu za kwenda wengine baadhi yenu wanaenda kwenye ziara fupi, lakini wengine wanaelekea majimboni nawatakia kila la kheri na tuonane tarehe ambayo ameitaja Mheshimiwa Waziri Mkuu na pengine mapema kabla ya hapo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mpaka tarehe 1 Novemba, 2022 saa tatu kamili asubuhi.

(*Saa 5.39 asubuhi Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne,  
Tarehe 1 Novemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi*)